SportPesa
TZS. 619,207,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Polisi:**
Uchunguzi wa mwili nabii waonyesha ulinyofolewa viungo
UKURASA 4




**Haaland sasa kufungia mwaka 2021 kitandani**
UKURASA 21


# Nipashe

Alhamisi Oktoba 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580747

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian


# Msaidizi wa Sabaya adai kumpatia siri Mbowe

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**VIDEO SABAYA BENKI YAWASILISHWA KORTINI**

OFISA TEHAMA wa Benki ya CRDB, Kanda ya Kaskazini, Geofrey Nnko (31), amedai walipokea barua ya kutoa taarifa...




Wafanyabiashara wa soko dogo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, wakiwa katika mkutano jana, kwa ajili ya kujadili hatima yao baada ya kutakiwa kuhama, ili kupisha ujenzi wa ghorofa. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Majaliwa azindua kampeni madawati 1,000 Benki Exim

UKURASA 4

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu, wakiketi katika moja ya madawati yaliyotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya Mkoa wa Lindi, kama sehemu ya kampeni ya ugawaji madawati 1,000 kwa shule za msingi katika mikoa mbalimbali nchini. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Telack na (kushoto) ni Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu. **NA MPIGAPICHA WETU**




## TMA yahadharisha uhaba mvua mikoa nyeti chakula

UKURASA 2

**MICHEZO** NABI: HESABU YANGA, AZAM PASUA KICHWA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA




Meneja Mkuu wa Kiwanda cha mabati cha ALAF, Paul Raj (wanne kulia), akimkabidhi Ofisa Mnadhimu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkadam Mkadam (kushoto), msaada wa mabati 500 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya kikosi hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Msaidizi Sabaya adai kutoa siri kwa Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MSAIDIZI wa zamani wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, Justine Kaaya, amedai alikutana na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, mara tatu na kumpa majina manane na namba za simu za marafiki wa Sabaya, akaahidi kushughulika nao.

Kaaya pia amedai alimtajia Mbowe klabu nne ambazo Sabaya alipenda kutembelea na hoteli tatu alizokuwa analala.

Shahidi huyo wa pili wa upande wa mashtaka alidai hayo jana Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavule, alidai alikuwa anafanya kazi na Sabaya tangu mwaka 2017 akiwa Diwani wa Kata ya Sambasha wilayani Arumeru, akipiga picha zake pamoja na viongozi wengine akiwamo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo.

Alidai alikuwa na kazi ya kupiga picha katika uchaguzi mdogo Jimbo la Longido na Sabaya alitaka amsaidie kupiga picha kwenye kata yake, alikubali akahama Longido kwenda Arusha nyumbani kwa Sabaya, eneo la Kibanda Maziwa, Sakina.

Alidai Sabaya alikuwa akiishi na mkewe Jesca katika nyumba hiyo na aliishi humo hadi Julai 2018, Sabaya alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai. "Nilienda kuishi na Sabaya katika makazi ya DC, Hai, nilikuwa msaidizi wake katika shughuli ndogo ndogo, kunyoosha nguo, kupeleka chai na chakula ofisini kila siku.

"Niliishi kwa Sabaya hadi Oktoba 2018 nikaamua kuacha kazi, nikarudi Longido kusimamia kazi zangu na niliacha mchumba.

"Novemba 2018 nilipigiwa simu na Mbowe kupitia namba yake 0784779944, alijitambulisha na kuomba tuonane, alisema yuko Arusha, nilimwambia niko Longido kuna changamoto ya usafiri.

"Aliniambia nichukue Noah atalipa gharama nikifika Arusha lakini nilikataa kwa sababu ya hofu, alikata simu, baada ya muda akapiga na kusema yuko njiani anakuja Longido. "Baada ya dakika 40, alinipigia kafika yuko uwanja wa mpira, nilienda kwa bodaboda, nikakuta gari, nikampigia akaniambia nisogee kwenye gari, nilipofika niligonga kioo, akashusha na kuniambia niingie ndani ya gari nisiwe na wasiwasi.

"Niliingia siti ya nyuma, ndani alikuwa Mbowe na dereva mwanamke, alisema Lengai anamsumbua, akataka nimpe taarifa za kazi anazofanya Sabaya na watu wake wa karibu alionao Hai.

"Nilimwambia haiwezekani sipo kwa Sabaya, alisema yeye kiongozi wa chama kikuu cha upinzani nchini, atafanya namna yoyote anayoweza ili nirudi kuendelea na kazi kwa Sabaya," alidai Kaaya.

Alidai alimwambia Mbowe hawezi kurudi kwa Sabaya, alichagua kufanya shughuli zake binafsi na Mbowe alimwomba msamaha kwa kumsumbua, akampa Sh.300,000, akasema watawasiliana.

"Nilimpigia Sabaya simu kumpa taarifa lakini hakupokea, nilimpigia Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, nilimweleza yote aliyoongea Mbowe, nikarudi nyumbani.

"Mbowe alinipigia tena Januari 2020 kwa WhatsApp kupitia namba zake, akataka tuonane Moshi, nilienda Moshi, akanielekeza nishuke Machame Road, nikae upande wa kulia, akaja na gari aina ya Land Cruser V8 yenye mlingoti na bendera ya Bunge, namba za gari zilikuwa KUE.

"Alishusha kioo cha gari akaniambia ingia kwenye gari, nyuma akashuka mtu mmoja akaniambia nipite, niliingia kwenye gari na baada ya dakika nane tulifika Aishi Hoteli Machame.

"Mbowe na mlinzi wake tulienda kukaa upande wa mgahawa, akataka tuzungumze muda mfupi, wana mkutano ndani ya jimbo, aliniruhusu niagize kinywaji au chakula, ilikuwa saa saba mchana.

"Aliniomba nimtajie rafiki zake Sabaya aliokuwa nao Hai, nilimtajia majina yao na namba za simu.

"Nilimtajia Japhet Bendera, Renatus Sibula, Mtoto wa Mkulima, Silveter Nyegu, Binti wa Kichaga, Mwalimu Dorine, Watson Malimwengu na Enock Kirigiti.

"Alisema atashughulika nao, akasema atanitumia chochote kwenye simu lakini hakufanya hivyo nikaamua kurudi Arusha, Julai mwaka 2020 alinipigia kwa WhatsApp akasema saa moja usiku atakuwa Moshi niende.

"Nilienda tukakutana Keys Hoteli, nilikuwa na dereva wake Willy pamoja na mlinzi wake baunsa baunsa, tulimsubiri alipotoka kwenye kikao tulielekea kwenye gari tukiwa naye pamoja na Mbunge wa Viti Maalum, Joyce Mukya," alidai.

Shahidi huyo alidai walienda Aishi Hotel, Mbowe akamwambia Joyce atangulie chumbani, wao wana kikao kifupi.

# TMA: Kutakuwa na upungufu wa mvua

**Na Faustine Feliciane**

MIKOA inayozalisha chakula kwa wingi nchini inatarajiwa kuwa na uhaba wa mvua kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka kuanzia Novemba mwaka huu mpaka Aprili mwakani.

Uhalisia huo unatokana na utabiri wa mvua uliotolewa jana na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ambao unaonyesha maeneo mengi ya mikoa yatapata mvua za chini ya wastani na wastani kwa baadhi ya maeneo. Mikoa hiyo inayotarajiwa kupata upungufu wa mvua ni Mbeya, Songwe, Ruvuma, Iringa, Rukwa, Katavi, Njombe, Lindi, Mtwara na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi kutokana na mifumo ya hali ya hewa, mvua za wastani mpaka chini ya wastani zinatarajiwa katika mikoa hiyo ikiwamo pia mikoa ya Kigoma, Tabora, Singida na Dodoma. "Hali ya sasa ya joto la bahari eneo la kati la Bahari ya Pacific iko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani katika nusu ya kwanza ya msimu, hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo inayosababisha mvua katika maeneo ya pwani ya magharibi," alisema Dk. Kijazi.

Alisema kutokana na hali hiyo inayotarajiwa kunaweza kutokea athari mbalimbali na kuwataka wananchi na mamlaka husika kuchukua tahadhari. Alisema katika sekta ya kilimo na usalama wa chakula kutokana na mvua za chini zinazotarajiwa kutakuwa na upungufu mkubwa wa unyevunyevu kwenye udongo na kuathiri ukuaji wa mazao, lakini kunatarajiwa kuwepo kwa visumbufu vya mazao kama mchwa, panya, viwavijeshi na wadudu wengine.

"Lakini wakulima wanashauriwa kupanda mazao na mbegu zinazokomaa kwa muda mfupi na zinazostahimili mvua chache kama vile mazao ya jamii ya mizizi na mazao ya bustani... mazao haya ni kama mihogo, viazi, mtama na mazao mengine yenye kustahimili mvua chache," alisema.

## Video Sabaya benki yawasilishwa kortini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

OFISA TEHAMA wa Benki ya CRDB, Kanda ya Kaskazini, Geofrey Nnko (31), amedai walipokea barua ya kutoa taarifa ya video ya kuonyesha tukio la aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akiingia tawi lao la Kwa Mrombo jijini Arusha.

Shahidi huyo wa saba wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Katika kesi hiyo, mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanaokabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Tersila Gervas, shahidi huyo alidai kuwa Mei 31 mwaka huu, alipokea taarifa kutoka kwa mkuu wake ikimtaka kufika kwenye tawi hilo ili kutoa video iliyorekodiwa kwenye kinasa picha (CCTV camera) kuhusu tukio la Januari 22 mwaka huu.

Alidai kuwa alipofika katika tawi hilo, walimkuta Meneja wa Tawi hilo, akiwa na maofisa wa TAKUKURU ambao ni Ramadhani Juma na Jonson Kisaka.

"Baada ya utambulisho huo walinionyesha barua ya kuomba video ya CCTV ya tukio lililotokea kwenye benki hiyo Januari 22 mwaka huu," alidai shahidi huyo na kuongeza kuwa aliwapa ushirikiano kufanikisha azma yao na alitia saini nyaraka kuthibitisha kutoa Wakili wa Utetezi anayewawakilisha washtakiwa wa tatu na wa nne, Fridolin Gwemelo, alipinga kupokewa kwa nyaraka hizo kortini kwa madai hakukuwa na cheti kinachoonyesha ubora wa mashine zilizotumika kurekodi tukio na kutoa taarifa hizo. Hata hivyo, pingamizi hilo lilitupwa.

**TAKUKURU**

Akitoa ushahidi wake Ofisa Maabara ya Uchunguzi wa Kielektroniki kutoka TAKUKURU, Jonson Kisaka (35), alidai kuwa Mei 31, 2021 alifika Arusha na kufanya uchunguzi wa video tajwa. "Tukiwa pale ndani (benki) nilimwomba Geofrey kunipatia matukio ya Januari 22, mwaka huu na baada ya kutafuta alizipata kutokana na kutafuta kwenye tarehe na muda husika," alidai shahidi huyo wa nane.

Alidai walijiridhisha kuwa ripoti hiyo ipo sawa baada ya kupitia na kuifungua video husika.

# TANGAZO

# TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA - NMB BANK PLC

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

NMB Karibu yako

Trilioni **8.2** Jumla ya Mali **+17%** YoY

Trilioni **6.1** Amana za Wateja **+18%** YoY

Trilioni **4.5** Mikopo Halisi Iliyopo **+13%** YoY

Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi **3.8%**

**Faida** kabla ya Kodi ya Mapato Bilioni **302** **+43%** YoY

**Faida** Baada ya Kodi ya Mapato Bilioni **211** **+42%** YoY

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi **47%**

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo Mwaka ya sasa 30.09.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.06.2021 | Robo Mwaka ya sasa 30.09.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.06.2021 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 472,717 | 405,346 | 472,717 | 405,346 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 867,924 | 1,008,328 | 867,924 | 1,008,328 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,477,857 | 1,345,548 | 1,477,857 | 1,345,548 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 413,592 | 157,223 | 413,592 | 157,223 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 39,517 | 10,259 | 39,517 | 10,259 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 2,878 | 1,045 | 2,878 | 1,045 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 32,951 | 47,642 | 32,951 | 47,642 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 4,465,222 | 4,229,306 | 4,465,622 | 4,229,706 |
| 12 | Mali Nyingine | 216,396 | 205,543 | 291,601 | 283,074 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 193,610 | 198,949 | 160,934 | 165,781 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **8,185,584** | **7,612,109** | **8,228,513** | **7,656,872** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 43,138 | 57,203 | 43,138 | 57,203 |
| 18 | Amana za Wateja | 6,051,740 | 5,843,527 | 6,053,622 | 5,845,671 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 142,797 | 80,489 | 142,797 | 80,489 |
| 20 | Amana Maalumu | 37,157 | 12,113 | 37,157 | 12,113 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,180 | 2,118 | 2,180 | 2,118 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 75,521 | 61,277 | 75,168 | 60,663 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | 40,571 | 37,994 | 40,571 | 37,994 |
| 27 | Dhima Nyingine | 69,215 | 66,175 | 114,787 | 112,482 |
| 28 | Madeni | 441,742 | 253,337 | 441,742 | 253,337 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **6,904,061** | **6,414,233** | **6,951,162** | **6,462,070** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,281,523** | **1,197,876** | **1,277,351** | **1,194,802** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,037,941 | 1,037,941 | 1,040,642 | 1,040,642 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 210,965 | 135,503 | 208,004 | 133,640 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 8,705 | 520 | 8,705 | 520 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,912 | 3,912 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,281,523** | **1,197,876** | **1,277,351** | **1,194,802** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,135,812 | 770,686 | 1,135,812 | 770,686 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 178,924 | 191,412 | 178,924 | 191,412 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 220,436 | 214,660 | 220,436 | 214,660 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 11,016 | 12,974 | 11,016 | 12,974 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 16% | 16% | 16% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.8% | 4.3% | 3.8% | 4.3% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75% | 74% | 75% | 74% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55% | 56% | 54% | 55% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 78% | 75% | 77% | 75% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 5% | 13% | 5% | 13% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 8% | 10% | 7% | 10% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Robo ya Mwaka sasa 30.09.2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 | Robo ya Mwaka sasa 30.09.2021 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 209,221 | 180,425 | 209,221 | 180,492 | 596,020 | 515,082 | 596,020 | 515,380 |
| 2 | Gharama za Riba | (34,806) | (37,826) | (34,806) | (37,826) | (98,162) | (104,740) | (98,162) | (104,740) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **174,415** | **142,599** | **174,415** | **142,666** | **497,858** | **410,342** | **497,858** | **410,640** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (30,034) | (32,554) | (30,034) | (32,554) | (83,073) | (80,999) | (83,073) | (80,999) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **82,730** | **70,932** | **82,730** | **70,932** | **222,646** | **189,978** | **222,646** | **189,978** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 9,628 | 7,164 | 9,628 | 7,164 | 22,495 | 18,636 | 22,495 | 18,636 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 68,936 | 61,104 | 68,936 | 61,104 | 184,923 | 162,391 | 184,923 | 162,391 |
| | 6.3 Gawio | 63 | - | 63 | - | 63 | 17 | 63 | 17 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 4,103 | 2,664 | 4,103 | 2,664 | 15,165 | 8,934 | 15,165 | 8,934 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(119,196)** | **(105,506)** | **(120,294)** | **(106,803)** | **(335,569)** | **(307,906)** | **(338,530)** | **(311,710)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (64,443) | (52,617) | (64,443) | (52,617) | (178,034) | (153,968) | (178,034) | (153,968) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (3,636) | (3,441) | (3,636) | (3,441) | (10,797) | (7,012) | (10,797) | (7,012) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (51,117) | (49,448) | (52,215) | (50,745) | (146,738) | (146,926) | (149,699) | (150,730) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **107,915** | **75,471** | **106,817** | **74,241** | **301,862** | **211,415** | **298,901** | **207,909** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (32,454) | (22,796) | (32,454) | (22,796) | (90,897) | (62,896) | (90,897) | (62,896) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **75,461** | **52,675** | **74,363** | **51,445** | **210,965** | **148,519** | **208,004** | **145,013** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | | | | | |
| | **Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa** | **8,185** | **799** | **8,185** | **799** | **7,913** | **(133)** | **7,913** | **(133)** |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **83,646** | **53,474** | **82,548** | **52,244** | **218,878** | **148,386** | **215,917** | **144,880** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,483 | 3,470 | 3,483 | 3,470 | 3,483 | 3,470 | 3,483 | 3,470 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 151 | 103 | 149 | 103 | 422 | 290 | 416 | 290 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 225 | 225 | 225 | 225 | 225 | 225 | 225 | 225 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 4% | 3% | 4% | 3% | 3% | 3% | 4% | 3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 24% | 20% | 24% | 20% | 22% | 19% | 23% | 19% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 46% | 49% | 47% | 50% | 47% | 51% | 47% | 52% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11% | 10% | 11% | 11% | 10% | 10% | 11% | 11% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI | | BENKI | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa 30.09.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.06.2021 | Robo Mwaka ya sasa 30.09.2021 | Robo Mwaka iliyopita 30.06.2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.09.2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30.09.2020 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 107,915 | 100,253 | 106,817 | 99,092 | 301,862 | 211,413 | 298,899 | 207,908 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 13,610 | 10,038 | 13,118 | 9,545 | 33,517 | 33,684 | 32,040 | 32,206 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (221,225) | (100,386) | (221,225) | (100,386) | (389,384) | (368,685) | (389,313) | (364,729) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 281,500 | 710,037 | 281,238 | 708,592 | 818,158 | 368,532 | 820,035 | 364,298 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 19,923 | 5,434 | 19,449 | 12,074 | (11,405) | 7,853 | (7,152) | 1,666 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (33,502) | (11,876) | (31,176) | (15,417) | (41,651) | 42,711 | (43,412) | 54,159 |
| - Kodi Iliyolipwa | (38,795) | (29,475) | (38,795) | (29,475) | (94,706) | (87,082) | (94,706) | (87,082) |
| - Mengineyo (bainisha) | (45,023) | (31,866) | (45,023) | (31,866) | (67,593) | 1,492 | (67,593) | 1,492 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **84,403** | **652,159** | **84,403** | **652,159** | **548,798** | **209,918** | **548,798** | **209,918** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (8,271) | (1,756) | (8,271) | (1,756) | (13,946) | (14,125) | (13,946) | (14,125) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (124,124) | (137,499) | (124,124) | (137,499) | (165,689) | (421,040) | (165,689) | (421,040) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(132,395)** | **(139,255)** | **(132,395)** | **(139,255)** | **(179,635)** | **(435,165)** | **(179,635)** | **(435,165)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (68,500) | - | (68,500) | (68,500) | (48,000) | (68,500) | (48,000) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 188,405 | (49,283) | 188,405 | (49,283) | 118,002 | (1,478) | 118,002 | (1,478) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **188,405** | **(117,783)** | **188,405** | **(117,783)** | **49,502** | **(49,478)** | **49,502** | **(49,478)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **140,413** | **395,121** | **140,413** | **395,121** | **418,665** | **(274,725)** | **418,665** | **(274,725)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,185,281 | 790,160 | 1,185,281 | 790,160 | 907,029 | 1,213,370 | 907,029 | 1,213,370 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **1,325,694** | **1,185,281** | **1,325,694** | **1,185,281** | **1,325,694** | **938,645** | **1,325,694** | **938,645** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **1,106,441** | - | - | **4,704** | **1,131,145** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 210,965 | - | - | - | 210,965 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 7,913 | 7,913 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,248,906** | - | - | **12,617** | **1,281,523** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **944,473** | - | - | **4,630** | **969,103** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 148,519 | - | - | - | 148,519 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (133) | (133) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,044,992** | - | - | **4,497** | **1,069,489** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **1,109,142** | - | - | **792** | **1,129,934** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 208,004 | - | - | - | 208,004 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 7,913 | 7,913 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (68,500) | - | - | - | (68,500) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,248,646** | - | - | **8,705** | **1,277,351** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **951,341** | - | - | **1,049** | **972,390** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 145,013 | - | - | - | 145,013 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (133) | (133) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,048,354** | - | - | **916** | **1,069,270** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA SEPTEMBA 2021

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna **Afisa Mtendaji Mkuu** | | Oktoba 22, 2021 |
| Juma Kimori **Afisa Mkuu wa Fedha** | | Oktoba 22, 2021 |
| Benedicto Baragomwa **Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | Oktoba 22, 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na PricewaterhouseCoopers, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede **Mwenyekiti wa Bodi** | | Oktoba 22, 2021 |
| Leonard Mususa **Mkurugenzi** | | Oktoba 22, 2021 |

www.nmbbank.co.tz

# Mwanasheria wa IPTL aachiwa kwa dhamana

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imemwachia kwa dhamana Mwanasheria wa Kampuni ya kufua umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), Joseph Makandege, anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000.

Mahakama hiyo chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, imetoa dhamana hiyo baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutoa masharti.

Mshtakiwa alitakiwa kuwa na wadhamini wawili watakatoa nusu ya fedha taslimu au hati ya mali zisizohamishika zenye thamani hiyo ya fedha anayodaiwa kusababisha hasara.

Wadhamini wawili wa Makandege waliwasilisha hati mbili za nyumba ya kwanza ikiwa na thamani ya Sh. milioni 398 na ya pili ya Sh. milioni 316 na kufanya thamani ya mali zote kuwa Sh. milioni 714.

Mbali na hati mshtakiwa ameamriwa kuwasilisha hati zake za kusafiria mahakamani na kwamba asitoke nje ya Jiji la Dar es Salaam bila kibali cha mahakama.

Awali, Wakili wa Serikali, Faraji Ngukah alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya dhamana.

Mapema mahakamani hapo Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), alimfutia mshtakiwa mashtarti ya kutakatisha fedha na mahakama ilimtaka kwenda Mahakama Kuu kuomba dhamana. Katika hati mpya ya mashtaka, mshitakiwa huyo anakabiliwa na kosa la kuisababishia hasara serikali ya Dola za Marekani 980,000.

Ilidaiwa kwamba, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu, kati ya Oktoba 18, 2011 hadi Machi 9, 2014, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshtakiwa huyo ambaye si mtumishi wa umma akishirikiana na watumishi wa umma, walitekeleza njama za hila ili kujipatia fedha.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kati ya Januari 23 hadi Februari 10, 2014 katika benki ya Stanbic, tawi la Kati, Wilaya ya Kinondoni na Benki ya UBL Ilala, Dar es Salaam, kwa nia ya udanganyifu, alijipatia kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dola za Marekani 380,000 na Dola 600,000.

Shtaka la tatu ni la kuisababishia Serikali ya Tanzania hasara kwamba katika tarehe hizo mshtakiwa huyo aliisababishia serikali hasara ya jumla ya Dola 980,000.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Hakimu alimtaka mshtakiwa huyo kutojibu mashtaka kwa kuwa mahakama hiyo haina Mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Novemba 4, mwaka huu na mshtakiwa yuko nje kwa dhamana.



Ofisa Msimamizi Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mercy Macha (kushoto), akimwelimisha mfanyabiashara wa soko kuu la Sumbawanga, kuhusu matumizi ya mashine za EFD na masuala ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT), wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango inayoendelea mkoani Rukwa jana.

# Majaliwa azindua kampeni ya madawati 1,000 ya Benki Exim

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua rasmi kampeni ya ugawaji madawati 1,000 yaliyofadhiliwa na Benki ya Exim Tanzania kwa ajili ya shule za msingi katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma, Mtwara, Lindi, Mbeya, Mwanza na Tanga.

Hatua hiyo inalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kukabiliana na uhaba wa madawati katika baadhi ya shule nchini sambamba na kuboresha sekta ya elimu.

Hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo ilifanyika mkoani Lindi na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo viongozi waandamizi wa serikali, baadhi ya wabunge wa mkoa wa Lindi, wananchi, wanafunzi pamoja na viongozi wa benki hiyo.

Akizungumza katika uzinduzi huo Majaliwa alisema pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa jitihada hizo, alisema hatua hiyio itasaidia sana katika kupinguza idadi ya wanafunzi wanaokabiliwa na ukosefu wa madawati, huku akibainisha kuwa kwa sasa serikali inaendelea na jitihada mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuimaliza kabisa changamoto hiyo.

"Jitihada hizi za Benki ya Exim zimekuja wakati mwafaka wakati pia serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya elimu katika kujenga vyumba vya madarasa nchini na kuboresha miundombinu ya elimu nchini, lengo ni kuhakikisha kwamba pamoja na ongezeko hili la wanafunzi kutokana na mpango wa elimu, lakini wanaketi kwenye madawati," alisema Waziri Mkuu Majaliwa

Katika hafla hiyo ilishuhudiwa Waziri Mkuu akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, madawati 200 kwa ajili ya mkoa wa huo ikiwa ni sehemu ya mpango huo, huku akiwaomba wadau mbalimbali kuiga mfano wa benki ya Exim kwa kujitokeza kwa wingi kuunga mkono jitihada hizo.

Awali akizungumza kuhusu kampeni hiyo Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Jaffari Matundu, alisema ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kusaidia jamii unaofahamika kama Exim Cares na dhamira ya benki hiyo katika kuisaidia serikali kukabiliana na upungufu wa madawati katika baadhi ya shule nchini.

"Uzinduzi wa kampeni hii muhimu unalenga kuunga juhudi za Serikali kuboresha miundombinu ya elimu nchini. Kampeni itahusisha utoaji wa madawati 1,000 katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dodoma, Mtwara, Lindi, Mbeya na Mwanza na ugawaji wake utazingatia hali ya uhitaji," alisema Matundu.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainabu Telack aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo, huku akiiomba iendelee kutazama pia sekta nyingine ikiwamo afya.

# Polisi wasema mwili wa nabii ulinyofolewa viungo

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha limetoa ripoti ya uchunguzi kuhusu kifo chenye utata cha Nabii Abraham Peter 'maarufu Katapila, likibainisha kuwa baada ya kuuawa viungo vyake vya siri vilivyofolewa.

Nabii huyo baada ya kuuawa Oktoba 14 mwaka huu, mwili wake ulitelekezwa na watu wasiojulikana, ukiwekwa lango la kuingilia Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Jastine Masejo, alisema nabii huyo alikwenda Arusha kwa ajili ya kutoa huduma ya maombi, akitokea jijini Dar es Salaam.

"Mpaka sasa tumeshawahoji watu wanne ambao ni wachungaji waliokuwa naye kabla ya umauti kumkuta. Huyu Nabii Abraham aliwasili Arusha Oktoba 12, mwaka huu," alisema.

Kwa mujibu wa jeshi hilo, Nabii Katapila ni mkazi wa Dar es Salaam na kiongozi wa kiroho aliyekwenda mkoani Arusha kutoa huduma.

Kamanda Masejo alisema kuwa nabii huyo na wachungaji hao awali walifanya maombi katika Mlima Duluti uliopo Wilaya ya Arumeru, Oktoba 14, mwaka huu na walirejea mjini Arusha na kupata mlo katika maeneo yaliyopo karibu na mlima huo.

Alisema kuwa baada ya kula, kila mmoja aliondoka na usafiri wake na kwamba Nabii Abraham alipokodi usafiri wa pikipiki kwenda kwa mchungaji mwenyeji wake alikokuwa amefikia jijini Arusha. Hata hivyo Kamanda Masejo hakutaja jina la mchungaji huyo.

"Baadaye usiku, mwili wake ulikutwa kwenye lango la Hospitali ya Mount Meru, ukiwa na majeraha yaliyosababishwa na kitu chenye ncha kali.

"Kifo chake ni cha utata kwa sababu haijajulikani kwa nini alitelekezwa kwenye mlango wa hospitali, huku mwili wake ukiwa na majeraha," alisema Kamanda Masejo. Kutokana na utata huo, Kamanda Masejo alisema bado wanafanya uchunguzi kubaini kama ni mauaji ya kupangwa au ajali.

Kamanda huyo alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kifo cha Nabii Abraham kilisababishwa na kuvuja damu nyingi.

Mwili wa Nabii Abraham umeshafanyiwa uchunguzi wa kitabibu na ndugu wa marehemu wameruhusiwa kuusafirisha kwenda Kitunda, Pwani. Nipashe ilizungumza na rafiki wa nabii huyo anayejulikana kwa jina la Master King Prophet John, ambaye alidai kifo cha Nabii Katapila kina utata.

Alisema marehemu alikuwa mmisionari ambaye hana kanisa na alikuwa akitoa huduma za kinabii katika kanisa lolote au kokote anakoitwa.

"Tumejiuliza kwamba ni vita vya watumishi hao waliomwita wakiodhani ana mali au ni ajali tu ya barabarani?" Alisema.

# TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### TANZANIA COMMERCIAL BANK

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|---|
| | | | 30/09/2021 | 30/06/2021 |
| A. | | MALI | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 41,873 | 42,425 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 64,413 | 67,804 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 112,814 | 115,988 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 78,327 | 88,611 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 435 | (35) |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 85,297 | 133,356 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 681,988 | 658,761 |
| | 12 | Mali Nyingine | 46,632 | 46,141 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,522 | 23,332 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,134,301** | **1,176,384** |
| B | | DHIMA | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| | 18 | Amana za Wateja | 755,420 | 754,781 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 156,088 | 212,906 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 1,300 | 5,730 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | 2 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 21,005 | 20,996 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,456 | 2,254 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 26,208 | 28,567 |
| | 28 | Madeni | 60,724 | 40,920 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,023,203** | **1,066,155** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **111,097** | **110,229** |
| C. | | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | - | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 66,533 | 66,533 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 8,402 | 7,534 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 8,090 | 8,090 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **111,097** | **110,229** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 171,250 | 224,141 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 94,680 | 82,434 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 24,238 | 21,900 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 83 | 27 |
| D. | | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.79% | 9.37% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.27% | 12.00% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 94.46% | 91.00% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.12% | 56.00% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.86% | 73.29% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 0.08% | 12.98% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -3.58% | 15.64% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO /MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30-Sep-21 | 30-Jun-21 | 30-Sep-21 | 30-Sep-20 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 3,057 | 7,520 | 15,093 | 18,462 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 5,895 | 4,151 | 17,496 | 16,241 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (23,227) | (4,037) | (64,175) | (206,905) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (56,179) | 200,207 | 119,591 | 265,134 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (8,357) | (21,004) | (9,313) | 76,313 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (490) | (29,896) | (4,812) | (30,757) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (2,189) | (2,552) | (6,690) | (5,249) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 46,995 | (29,015) | (95,484) | (77,032) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(34,495)** | **125,374** | **(28,294)** | **56,208** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,361) | (1,872) | (4,824) | (2,568) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(1,361)** | **(1,872)** | **(4,824)** | **(2,568)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,694) | (1,226) | (5,432) | (4,553) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(2,694)*** | ***(1,226)*** | ***(5,432)*** | ***(4,553)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (38,550) | 122,276 | (38,550) | 49,087 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **173,727** | **51,451** | **173,727** | **23,959** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 135,177 | 173,727 | 135,177 | 73,046 |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 30-Sep-21 | 30-Sep-20 | 30-Sep-21 | 30-Sep-20 |
| 1 Mapato ya Riba | 33,720 | 35,163 | 99,075 | 89,420 |
| 2 Gharama za Riba | (9,762) | (11,474) | (29,008) | (27,495) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **23,957** | **23,689** | **70,067** | **61,925** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (72) | (37) | (157) | (359) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,398) | (793) | (10,339) | (5,328) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **6,559** | **6,486** | **25,071** | **20,896** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,338 | 1,799 | 3,925 | 3,741 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,615 | 4,012 | 13,329 | 10,660 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 606 | 674 | 7,817 | 6,495 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(23,989)** | **(22,827)** | **(69,549)** | **(58,673)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 11,958 | 11,048 | 34,417 | 28,479 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 933 | 1,264 | 3,355 | 3,744 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 11,098 | 10,516 | 31,778 | 26,449 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,057** | **6,518** | **15,093** | **18,462** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 2,189 | 1,700 | 6,690 | 5,249 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **869** | **4,818** | **8,402** | **13,214** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **869** | **4,818** | **8,402** | **13,214** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,103 | 1,049 | 1,103 | 1,049 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 31 | 172 | 299 | 471 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 47 | 44 | 47 | 44 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.08% | 0.45% | 0.77% | 1.57% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.77% | 3.88% | 7.71% | 11.79% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 59.56% | 54.81% | 56.02% | 53.19% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.64% | 2.80% | 8.12% | 9.02% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 8,402 | **8,402** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | (1,604) | **(1,604)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | **-** | **66,533** | **(0)** | **0** | **16,492** | **111,097** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **60,601** | **(0)** | **0** | **10,220** | **98,893** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 5,866 | - | - | - | **5,866** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 66 | - | - | - | **66** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | (526) | **(526)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | **-** | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA, 2021

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | Imesainiwa | **18.10.2021** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | Imesainiwa | **18.10.2021** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | Imesainiwa | **18.10.2021** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | Imesainiwa | **18.10.2021** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI** Mjumbe wa Bodi | Imesainiwa | **18.10.2021** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usifanyike mzaha katika kupata wataalamu wa afya

**OKTOBA** 15, mwaka huu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ilitangaza matokeo ya mitihani ya utabibu.

Katika taarifa yake, ilieleza kuwa matokeo yote ya wanafunzi wa ngazi ya tano ya programu ya utabibu yamezuiwa hadi taarifa ya uchunguzi kutoka wizara hiyo itakapokamilika na kuwasilishwa NACTE kwa ajili ya maamuzi.

Wanafunzi takribani 35 kutoka vyuo mbalimbali walifutiwa matokeo yao na kusimamishwa kuendelea na masomo kwa tuhuma za kufanya udanganyifu kwenye mitihani.

Tayari wizara hiyo imeshasema, Jumatatu ijayo itaweka wazi watu wote waliohusika na uvujaji wa mitihani ya utabibu nchini.

Kwamba, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kuhusika na uvujaji huo na kubainisha kuwa wizara imeshaunda kamati itakayoandaa ripoti na kuikabidhi kwake na anatarajia kuisoma kwa umma.

Tunaishukuru serikali kwa kuchukua hatua za kufanya uchunguzi, ili ukweli ujulikane kuhusiana na tuhuma hizo, hasa kutokana na ukweli kwamba, taaluma hiyo inahusu afya za watu.

Kimsingi suala la afya ni nyeti, hivyo ni vyema wanaosomea taaluma hiyo wakafaulu kulingana na uwezo wao wa darasani, ndiyo maana tunaishukuru serikali kufanya uchunguzi ili kujua ni nini kimetokea hadi mitihani ikavuja.

Hatua hiyo ya kufanya uchunguzi, inaonyesha ni jinsi gani serikali haitaki kuona mtu yeyote anaonewa kwenye sakata hilo, bali ukweli ujulikane ili kuondoa sintofahamu ambayo inaweza kusababishwa na uvujaji wa mitihani.

Kwa kuwa kinachoelezwa ni tuhuma, nasi tunaona ipo haja kukumbusha kuwa elimu ya taalum ya afya inahusu uhai wa Watanzania, ambayo ni vyema wanaoisomea wakihitimu kulingana na uwezo wa akili zao. Tunaamini kwamba, bila mtu kuhitimu vizuri masomo ya utabibu, anaweza kusababisha madhara ya kiafya kwa Watanzania, kwa sababu ya kufaulu kwa kutumia mitihani iliyovuja au njia nyingine za kughushi ambazo hazikubaliki.

Lakini kama atakuwa amefanya mitihani na kufaulu, tunadhani kuwa huyo anaweza kuwa msaada mkubwa kwenye jamii inayomzunguka au katika eneo la kazi ambalo atakuwa amepangiwa.

Kama anavyosema Waziri mwenye dhamana ya Afya za Watanzani, Dk. Dorothy Gwajima, kwamba vyuo vya kada ya afya vinatarajiwa kutoa watumishi watakaokuja kuwahudumia Watanzania nasi tunakubaliana na hilo.

Ni kweli kwamba kitendo cha kuwapatia watu majibu ya mitihani bila kufanya na kufaulu mitihani ni sawa na kwenda kuhatarisha afya za Watanzania kwa kufanya kazi ambayo hawakuihitimu inavyotakiwa.

Tunashauri kuwekwa kwa mifumo bora katika kuwaingiza watu katika utumishi kwenye sekta ya afya kuanzia vyuoni na pia kuendelea kuwafuatilia hata baada ya kuajiriwa kuhusu uwezo wao wa kitaaluma kuepusha uwezekano wa kudhuru maisha ya watu.

Tunaamini kuwa hili litawekwa bayana kwa muda mwafaka, ili umma uelewe hatua zitakazochukuliwa na kuwa funzo kwa wengine.

Katika kuhakikisha kwamba taaluma hii haichezewi, tunaona kwamba kuna umuhimu mkubwa kwa mamlaka zetu kuchukua hatua za makusudi wa kuwaondoa katika vyuo vya utabibu, uuguzi na udaktari watakaobainika kufanya vitendo vya udanganyifu.

Pia kuwaondoa watumishi walioajiriwa kwa njia zisizo halali. Lengo ni kulinda hadhi na heshima ya taaluma hiyo kwa jamii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mtihani darasa la nne inaanza, ikiisha wazazi tusijisahau sana

Na Adam Fungamwango

**WANAFUNZI** wa shule za msingi Tanzania wanaosoma darasa la nne, leo wanatarajiwa kufanya mtihani kwa ajili ya kusaka nafasi ya kufuzu kwenda darasa la tano.

Kwa elimu ya Tanzania, kwa sasa kama mwanafunzi atapata chini ya zile alama zilizowekwa, ni kwamba hawezi kwenda darasa la tano, badala yake atarudia tena mwaka unaofuata.

Hii ilitumika zamani wakati ule wa mkoloni na miaka kadhaa baada ya Uhuru, lakini baadaye mwanafunzi alikuwa akianza la kwanza hadi la saba b ila kukatizwa.

Aelewe, asielewe yeye anakwenda hadi la saba, ilikuwa na manufaa yake na serikali ilikuwa na nia nzuri. Baadaye mambo yakabadilika. Ndipo wakaanza kupatikana wanafunzi wanaomaliza darasa la saba, bila ya kujua kusoma na kuandika, achilia mbali kuhesabu.

Serikali ikaona irudishe utaratibu wa mwanafunzi akifika la nne afanya mtihani wa Taifa kwa ajili ya kufuzu kuingia la tano. Lengo lilikuwa kuwafanya watoto kukazana kusoma na kuwasilikiza walimu wao kwa sababu alione, akiwa mzembe ataendelea kusota la nne.

Walimu nao wakakazana kuwafundisha wanafunzi wasije kuonekana hawafanyi kazi zao vema. Wakawa wanajitahidi kusiwe na mwanafunzi 'mbumbumbu', ambae ataendelea kusota darasa la nne kwa angalau mwaka mmoja.

Wazazi nao wakawa makini kwa watoto wao. Wakawa wanapeleka tuisheni wakirejea kutoka shuleni, lakini kuna wazazi ambao wanaweza kuwafundisha watoto wao, wakawa wanafanya hivyo ili kuwafanya asikwame kati, kwenye darasa la nne.

Nawatakiwa kila la kheri wanafunzi wote wa Tanzania kwa mtihani wanaokwenda kufanya na wawe na mafanikio. Ila jambo moja nataka niwakumbushe wazazi wa wanafunzi.

Kumaliza kufanya mtihani wa darasa la nne siyo kumaliza shule. Nasema hivi, namaanisha. Nimekuwa nikiona, baada ya wanafunzi kufanya mitihani, wanarejea nyumbani na kuishi kana kwamba hawatorejea tena shuleni.

Sina maana kwamba mtoto asisafiri au kwenda kutembelea ndugu, ila aende mara moja na kurejea kujipanga na masomo ya darasa la tano.

Huu siyo wakati ambao mtoto ameshafanya mtihani, basi anapelekwa kukaa kwa bibi, babu, shangazi, mjomba hadi matokeo yanatoka, mpaka siku mbili au ndiyo anarudi, kabla hajajiandaa na chochote kile anaanza shule darasa la tano.

Baadhi ya wazazi wanadhani sasa huu ndiyo wakati wa kuwatumikisha kwenye biashara ambazo ama wanazozianzisha, au walizokuwa wakizifanya wao.

Utaona mwanafunzi kwa sababu ameshafanya mtihani anasubiri majibu, anapita barabarani anauza mboga za majani, mahindi, mihogo au anawekwa gengeni kuuza nyanya, vitunguu na vitu vingine. Huu siyo wakati wake.

Mtoto anatakiwa apumzike nyumbani. Awe anawasaidia wazazi kazi ndogondogo za nyumbani, kama kupika, kufua, kupiga kazi, kufuga, lakini siyo kuzurura barabarani na mabeseni ya vitu vya kuuza.

Huko ni kumdumaza mtoto kielimu, kwani akianza darasa la tano anakuwa kama anaanza upya la kwanza. Ni wakati wa kumpumzisha mtoto na safari za miaka minne za shule, pia akinoa ubongo wake kwa kile ambacho atakwenda kukikuta darasa la tano atapoanza, ili asiwe mgeni sana, au kuona masomo magumu.

Na kwa watoto pia, wanapomaliza kufanya mitihani wasione kama wamemaliza na kuanza michezo isiyo na faida ya kuzunguka kwenda kwa rafiki fulani na fulani.

Michezo wanayotakiwa kucheza ni ile ya kawaida ya shuleni kama mpira wa miguu, mikono, pete, wavu, lakini huku pia wakizingatia masomo.

Na si ile ya kutembea kutwa nzima, tena bila kuaga nyumbani, haijulikani wanakwenda wapi, huku wazazi wakiwa wanawatafuta nyumbani.

## Mabilioni IMF kutatua kero ukosefu wa maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amesema Sh. bilioni 139.4 za sekta ya maji kati ya Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), zinatarajia kuboresha miradi ya maji maeneo mbalimbali ya nchi.

Fedha hizo zilitolewa na IMF ikiwa mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mapambano dhidi ya corona.

Katika fedha hizo, Aweso amesema Sh. bilioni 104.2 zinalenga kuboresha utekelezaji wa miradi 218 ya maji mijini na vijijini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Aweso alisema miradi 46 itatekelezwa mijini huku miradi 172 ikiwa ya vijijini ili kuhakikisha kila mmoja anapata maji ya kutosha.

Pia alisema Sh. bilioni 17.6 zitatumika kununua mitambo ya ujenzi wa mabwawa na vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi.

"Pia Sh. bilioni 17.5 zitatumika kununua seti 25 za mitambo ya kuchimbia visima ambapo kila mkoa utapata mtambo mmoja," alisema.

Aweso alisema wizara yake itahakikisha mitambo hiyo inatunzwa na kutumika ilivyokusudiwa ili iweze kutumika kwa muda mrefu na kwamba utekelezaji wa miradi hiyo utasaidia wananchi milioni mbili kupata maji.

Aliagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), bodi za maji za mabonde kuhakikisha fedha hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa kwa manufaa ya taifa.

"Mimi na viongozi wengine wa wizara tutafuatilia kuhakikisha fedha hizo zinafanya kazi yake kikamilifu," alisema.

Kuhusu mitambo ya kuchimba visima, alisema watakuwa wakifanya utafiti kabla ya kuchimba kupitia vifaa ambavyo watavinunua ili kuepuka kupata hasara.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa maji, wamepanga kununua seti nne za vifaa vya kisasa kwa utafiti wa maji chini ya ardhi.



Baadhi ya wafanyakazi wa Barrick North Mara, wakiwa pamoja na watoto wanaolelewa katika kituo cha yatima cha Angel House wilayani Tarime, mkoani Mara hivi karibuni, baada ya kukabidhi msaada wa chakula uliotolewa na kampuni hiyo, katika kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Marekani yasaidia TEC mapambano corona

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kitaifa (USAID) imetoa Dola za Marekani 550,000 (Sh. bilioni 1.3) kwa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC) kutekeleza mradi wa 'Pambana na Uviko-19' kwa madhumuni ya kuunga mkono juhudi za kitaifa za kukabiliana na janga la Uviko-19.

USAID na TEC wamezindua mradi huo mpya wa kuimarisha uwezo wa vituo vya afya, watumishi wa afya, viongozi wa dini na watu wenye ulemavu kukabiliana na janga hilo nchini.

Hafla ya uzinduzi wa mradi wa 'Pambana na Uviko-19' ilifanyika jana jijini Dar es Salaam, ikihudhuriwa na Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddaeus Ruwai'chi, Rais wa Baraza la Maaskofu na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu.

Balozi Wright alisema Serikali ya Marekani kupitia USAID imetoa dola hizo kwa madhumuni ya kuunga mkono juhudi za kitaifa za kukabiliana na janga la Uviko-19, kuwezesha ununuzi wa vifaa vya matibabu kama vile mitungi ya oksijeni, vifaa vya ufuatiliaji wa wagonjwa na mashine ndogo za kutengeneza oksijeni katika hospitali 12 za Dar es Salaam, Kagera, Bukoba, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Arusha, Kilimanjaro, Singida, Mtwara na Iringa.

Alisema mradi wa 'Pambana na Uviko-19' utaongeza ujuzi wa wafanyakazi wa afya ili kuboresha usimamizi wa wagonjwa na kusaidia usimamizi wa chanjo katika mikoa 12 pamoja na miongozo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Rais wa TEC, Askofu Gervas Nyaisonga, alisema Kanisa Katoliki litaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Uviko-19 ili kuendeleza kuinusuru jamii.

"Matamanio yetu ni kuhakikisha kwamba corona haienei na inatoweka kwenye jamii ndiyo maana baada ya kuona hili 'gonjwa' linaendelea kuenea, tuliamua kwenda watu wa Marekani kupitia USAID, na hatimaye tukaweza kusaidiwa vifaa katika hospitali 12 za nchini.

"Tunaipongeza USAID kwa kuunga mkono uhamasishaji wa chanjo ya Uviko-19 katika kuokoa maisha ya watu. Mradi huu utahakikisha watu wengi wanapata elimu sahihi na kupata chanjo," alisema.

Waziri Mkuu aliishukuru Marekani kwa kuendelea kuisaidia Tanzania katika nyanja mbalimbali, akisisitiza kuwa taifa hilo kubwa kiuchumi, limefanya mambo mengi ya maendeleo nchini.

SPYTECH Security Supplies ltd

SPYTECH AUCTION MART & COURT BROKERS

NIC LIFE HOUSE BUILDING, SOKOINE DRIVE ROAD THIRD FLOOR, P.O.BOX 75602 DAR ES SALAAM
MAFINGA P.O.BOX 480 / MOB: +255 755 815 974 / +255 658 815 974
MBARALI MBEYA P.O.BOX 46

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TANGAZO HILI LIMETOLEWA LEO TAREHE 28/10/2021

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MUCOBA **BANK PLC-MAFINGA** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA MUCOBA BANK PLC-MAFINGA. MNADA UTAFANYIKA **TAREHE 4/12/2021** SIKU YA JUMAMOSI NA KUENDELEA KUANZIA SAA 4:10 ASUBUHI MPAKA 10:30 JIONI MAHALI ZILIPO DHAMANA ZA WADAIWA.

ORODHA YA WADAIWA NI KAMA WAFUATAO:

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALA ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|
| KIHANAGA WOMAN SACCOS | NYUMBA | MAFINGA - KINYANAMBO (A) |
| STEPHEN AIDAN MOSHA | NYUMBA NA KIWANJA | MAFINGA - MJINI |
| ABDALLAH MSAFIRI NZINGO | NYUMBA | MAFINGA - BLOCK (J) |
| JACKSON MGIMWA | NYUMBA | KINYANAMBO - AMANI |
| MAHMOUD HASSAN MGIMWA | NYUMBA | KINYANAMBO - AMANI |

NB: MASHARTI YA MNADA

MNUNUZI ATAKAE BAHATIKA ATATAKIWA KULIPA 25% YA BEI ILIYOFIKIWA PAPO HAPO. NA KIASI KILICHOBAKI CHA 75% KILIPWE NDANI YA SIKU 14, KINYUME NA HAPO PESA ILIYOTOLEWA AWALI HAITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA TENA. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI MILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE NA GHARAMA ZA KWENDA KUANGALIA/KUKAGUA NYUMBA SHAMBA/VIWANJA NI ZA MTEJA MWENYWE. IKUMBUKWE KUWA MDHAMINI NI SEHEMU YA MKOPAJI. LIPA DENI LAKO KABLA YA 28/11/2021 UKISUBILI MPAKA SIKU YA MNADA GHARAMA ZITAONGEZEKA TSHS 100,000/= **Wasiliana nasi kwa Namba 0755815974/0623815974**

WOTE MNAKARIBISHWA

# Katibu Mkuu awashukia watendaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** KONGWA

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, amewajia juu watendaji wa ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma na kuwataka kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na weledi.

Makondo alitoa kauli hiyo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza katika ofisi ya ardhi za halmashauri hiyo kutokana na kuwapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuwa kuna baadhi ya watumishi wa wanaodai fedha wakati wa kutoa huduma.

Alisema wizara haitasita kuchukua hatua kali kwa mtumishi yeyote wa ardhi atakayebainika kuwadai fedha wateja kinyume cha gharama halisi zilizowekwa na serikali kwa kisingizio cha fedha ya usafiri.

Kwa mujibu wa Makondo, ofisi yake ilipokea taarifa kutoka kwa mwananchi mmoja akidai kutakiwa kutoa fedha kwa ajili ya usafiri wa kufuatilia hati jambo alilosema halikubaliki kwa kuwa ni kuwatesa wananchi.

"Tunafuatilia kwa karibu wale wote wanaodai fedha kutoka kwa wateja maana hamjawekwa hapa kuwakandamiza wananchi na suala hili halikubaliki," alisema.

Makondo alisema wizara katika kuboresha huduma zake, iko mbioni kukamilisha Kituo cha Huduma kwa Wateja (Call Center) ambacho kitatumika kupokea changamoto na kero kutoka kwa wateja.

"Dhamana mliyopewa ninyi watumishi wa sekta ya ardhi ni 'privilege' maana ardhi inamhusu kila mtu. Kwa hiyo mnatakiwa kuangalia namna bora ya kutekeleza malengo ya wizara kwa weledi," alisema.

Akiwa katika wilaya ya Kongwa, Makondo alipata pia fursa ya kusalimia kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa na kuwaomba madiwani kushirikiana na ofisi ya ardhi kuhakikisha vijiji ndani ya wilaya hiyo vinapangiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi sambamba na kuongezwa kasi ya utoaji hati za kimila.

Wilaya ya Kongwa ina vijiji 87 na kati ya hivyo ni vijiji 41 ndivyo vyenye mpango wa matumizi bora ya ardhi na kufanya vijiji 46 kusalia kupangiwa mpango huo.

Kwa mujibu wa Makondo, wizara kwa sasa iko kwenye hatua za kukamilisha miradi yake mikubwa miwili ya Benki ya Dunia na mkopo wa Benki ya Exim kwa lengo la kuhakikisha ardhi ya Tanzania inapangwa na kupimwa na kufikia malengo ya kutoa hati 2,500,000 katika kipindi cha miaka miwili.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, ambaye ni Mbunge wa Kongwa, alimshukuru Katibu Mkuu kwa uamuzi wake wa kuitembelea wilaya hiyo kwa lengo la kutatua changamoto zilizojitokeza.

Hata hivyo, Ndugai aliweka wazi kuwa moja ya changamoto kubwa kwenye wilaya hiyo ni mashtaka yanayohusiana na migogoro ya ardhi, hivyo kuiomba wizara kuangalia namna ya kuipatia wilaya hiyo Baraza la Ardhi la Wilaya ili kuwaondolea usumbufu wananchi kufuata huduma Dodoma mjini.

# TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 11,504 | 13,251 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 10,969 | 21,904 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 30,000 | 29,000 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 11,987 | 3,999 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 48 | 88 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 23 | 18 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 74,770 | 73,106 |
| 12 | Mali Nyingine | 13,202 | 12,905 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 17,170 | 18,135 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **169,712** | **172,443** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 624 | 606 |
| 18 | Amana za Wateja | 120,665 | 121,946 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 23 | 25 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 1 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,503 | 3,757 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazo | 8,621 | 8,500 |
| 27 | Dhima Nyingine | 12,099 | 12,750 |
| 28 | Madeni | 403 | 690 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **146,938** | **148,276** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **22,774** | **24,16** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 22,411 | 22,411 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (5,416) | (6,852) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (5,512) | (4,298) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,291 | 12,906 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **22,774** | **24,167** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 68 | 61 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 12,254 | 15,996 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,018 | 8,904 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 13.4% | 14.0% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14.9% | 19.0% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 66.1% | 66.8% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 48.4% | 48.7% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 68.8% | 61.5% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.0% | 2.8% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -1.6% | 1.6% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.09.2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-21 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (1,214) | (1,694) | (5,512) | 262 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 567 | 596 | 1,793 | 645 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,664) | 465 | 2,933 | (5,463) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (1) | 0 | (1) | 0 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,266) | 3,344 | 1,497 | 4,721 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (1,000) | (3,150) | (7,230) | 450 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 602 | 1,337 | 4,249 | 272 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (298) | (1,060) | (1,893) | 225 |
| - Kodi Iliyolipwa | (135) | (124) | (157) | (7) |
| - Mengineyo (bainisha) | 577 | (222) | 1,142 | 419 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(3,831)** | **(509)** | **(3,178)** | **1,522** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (69) | (121) | (267) | (20) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(68)** | **(121)** | **(266)** | **(20)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (17) | (0) | (17) | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (677) | (65) | (1,132) | (586) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(694)** | **(65)** | **(1,149)** | **(586)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (4,593) | (696) | (4,593) | 916 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 31,972 | 32,668 | 31,972 | 17,248 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **27,379** | **31,972** | **27,379** | **18,164** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(5,626,989)** | **3,683,694** | **0** | **16,992,072** | **28,465,109** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (5,512,197) | 0 | 0 | 0 | **(5,512,197)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 11,426,798 | 5,386,179 | 0 | 0 | 0 | (16,992,072) | **(179,095)** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 210,589 | (210,589) | 0 | 0 | **(0)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2021** | **22,411,214** | **7,818,096** | **(10,928,597)** | **3,473,105** | **0** | **(0)** | **22,773,818** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **0** | **0** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (3,441,795) | 0 | 0 | 0 | **(3,441,795)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (4,101,254) | 4,101,254 | 0 | 0 | **(0)** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.09.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(2,855,410)** | **7,388,198** | **0** | **0** | **17,949,120** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2021
**(Kiasi kwa shilingi milioni)**

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-21 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 6,031 | 6,086 | 17,846 | 18,471 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,059) | (1,783) | (6,408) | (5,491) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **3,972** | **4,303** | **11,439** | **12,980** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (598) | 489 | (2,587) | (1,886) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,472** | **1,551** | **4,025** | **4,021** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 151 | 85 | 304 | 219 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 837 | 975 | 2,529 | 2,776 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 484 | 492 | 1,192 | 1,027 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,060)** | **(6,081)** | **(18,389)** | **(18,557)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,288) | (3,301) | (9,444) | (9,883) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (2,772) | (2,780) | (8,945) | (8,674) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,214)** | **262** | **(5,512)** | **(3,442)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,214)** | **262** | **(5,512)** | **(3,442)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,214)** | **262** | **(5,512)** | **(3,442)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 406 | 417 | 406 | 417 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (54) | 24 | (246) | (313) |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.8% | 1% | -4.3% | -3% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -20.7% | 6% | -31.3% | -26% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 111.3% | 104% | 118.9% | 109% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 14.3% | 17% | 13.7% | 17% |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.09.2021

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

**Jina na Cheo** | **Saini** | **Tarehe**

Silvest Arumasi
**(Mkurugenzi Mtendaji)**


Bertha Simon
**(Mkuu wa Fedha)**

Chemo Mutani
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Jina** | **Saini** | **Tarehe**

1. **Ernest Massawe**
2. **Dr. Josephat Daniel Lotto**

HUDUMA KIGANJANI

LIPIA LUKU, VING'AMUZI, MALIPO YA SERIKALI (GePG) BILA GHARAMA YA ZIADA KWA KUTUMIA AKIBA MOBILE

Piga *150*10#
Au
Pakua Akiba Mobile App

# Mulamula: Ushirikiano na Marekani ni wa faida

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya Tanzania imekiri kuwa uhusiano mkubwa wa miaka 60 kati yake na Marekani umeleta matokeo makubwa na ya kihistoria katika maeneo mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo mkoani Dar es Salaam wakati akifungua mkutano maalum uliojulikana kama 'Pamoja 60 Conference'.

Mkutano huo ambao uliandaliwa kwa ushirikiano baina ya Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini (REPOA) na Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania, uliangazia mafanikio ya ushirikiano wa nchi hizo kwa miaka 60 iliyopita.

Balozi Mulamula akihutubia kwa njia ya mtandao kupitia video iliyorekodiwa, alisema dhamira ya Tanzania ni kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Marekani na kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo ambao uliimarishwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na John Kennedy wa Marekani.

Alisema maadhimisho hayo ya miaka 60 yanashuhudia hatua nyingine muhimu katika urafiki huo wa kihistoria kwa pande zote mbili.

"Tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961, Marekani imekuwa ikisaidia juhudi za Tanzania za maendeleo katika sekta ya elimu, afya, maji, kilimo, demokrasia na haki za binadamu, miundombinu na teknolojia.

"Tunashukuru kwa Wamarekani ambao wamefanya kazi bila kuchoka katika maeneo ya mbalimbali hasa katika sekta za elimu na afya. Marekani imekuwa ikileta wafanyakazi wa kujitolea kufanya kazi katika sekta mbalimbali za afya, elimu, kilimo na nyingine. Tunashukuru kwa maono ya Mwalimu Nyerere na Kennedy," alisema.

Alisema katika kuhakikisha misaada inayotolewa na Marekani inaendelea kuwanufaisha Watanzania kwa sasa na baadaye, serikali inahakikisha inaimarisha demokrasia na haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na uhalifu wa kupangwa pamoja na kuimarisha amani na umoja.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema ziko programu mbalimbali katika vyuo ambavyo vinashirikiana na vya Marekani katika kuvijengea uwezo katika utafiti katika sekta ya afya, uchumi na nyingine.

Alisema REPOA ni miongoni mwa taasisi ambazo zimenufaika na uhusiano kati ya nchi hizo mbili ambapo baadhi ya watafiti wake wamepata elimu nchini Marekani.

Pia alisema wamekuwa wakifanya programu ambazo serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la USAID, limekuwa likitoa fedha kuwezesha kufanyika kwa tafiti mbalimbali.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright, alisema kama ilivyo kwa miaka 60 iliyopita, Marekani inaendelea na dhamira yake ya kushirikiana na serikali ya Tanzania kuimarisha sekta ya elimu kote nchini.

Alisema kwa miaka mitano pekee, Marekani kupitia shirika lake la USAID limechangia zaidi ya Dola za Marekani milioni 65 kwenye mfumo wa elimu ya msingi.

"Kwa mwaka 2020 pekee, mpango wa elimu wa USAID/Tanzania ulifikia takriban wanafunzi milioni 2.5 na uboreshaji wa mafunzo darasani; ilichapisha na kusambaza zaidi ya vitabu milioni 2.8 vya kusoma kwa darasa la awali na nyenzo za usaidizi za walimu na kutoa mafunzo kwa walimu 20,261 kutoka shule 3,074 katika mikoa iliyolengwa," alisema.

Pia alisema wanaunga mkono mfumo wa elimu ya sekondari ili kuongeza ushiriki wa watoto wa kike kubaki shuleni ambapo mpaka sasa msaada wa nchi hiyo umefikia karibu wanafunzi 50,000, walimu 1,300 na wazazi na walezi 6,000.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Shule za Tusiime, Dk. Albert Katagira, wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa tatu wa Chama cha Wawekezaji Binafsi katika Elimu (TAPIE), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Vijana wa mazingira magumu kukopeshwa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, inakusudia kuwasaidia kwa mikopo vijana wanaotoka kwenye mazingira magumu.

Vijana hao wameibuliwa na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) chini ya Taasisi ya Foxes Community and Wildlife Trust.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Deograsia Liganga, alisema kwa kupitia mradi huo, vijana hao wataweza kubadili maisha yao kiuchumi.

Akizungumza katika Kijiji cha Igoda wakati wa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wa kata tatu za Luhunga, Mdabulo na Ihanu ambao wanapatiwa mafunzo mbalimbali yakiwamo ya ujasiriamali, alisema Halmashauri ya Mufindi itaendelea kuwasaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupata mikopo kupitia fedha za makusanyo yake ya ndani.

Kwani alisema halmashauri kupitia fedha za makusanyo ya ndani imekuwa ikitenga asilimia 10 kwa ajili ya vijana asilimia 4, wanawake asilimia 4 na watu wenye ulemavu asilimia 2, hivyo iwapo watajiunga vikundi ni rahisi kunufaika na mikopo hiyo isiyo ya riba.

"Tunatambua jitihada kubwa zinazofanywa na mradi wa huu wa YAM ndani ya Halmashauri ya Mufindi na tunazidi kuwaomba kuendelea kuwasaidia vijana na watu wenye ulemavu," alisema.

Alisema mradi huo unaotekelezwa na YAM kupitia Taasisi ya Foxes pia halmashauri imekuwa mshiriki katika utekelezaji wake.

Aliwataka vijana wanufaika wa mradi huo kutumia vizuri fursa hiyo kwa kwenda kujiunga vikundi na kupitia vikundi wabuni miradi ili kuomba mikopo kwenye Halmashauri kukuza mitaji yao.

Meneja wa mradi wa YAM, Danford Mkumba, alisema vijana zaidi ya 690 wamelengwa kufikiwa na mradi huo utakaotekelezwa kwa miaka minne kuanzia mwaka huu.

Alisema kupitia mradi huo watoto wenye ulemavu zaidi ya 71 watanufaika na mradi huo.

# Madiwani wakunwa utendaji wa Samia

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MADIWANI wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya vizuri kwa muda mfupi kwenye maendeleo.

Miongoni mwa mambo aliyofanya vizuri wamesema ni kupeleka fedha kwa ajili ya kujenga madarasa 59 katika shule mbalimbali, jambo ambalo halikuwahi kutokea katika mkoa huo.

Akizungumza juzi wakati wa kufunga baraza la nne la madiwani, Meya wa Manispaa ya Mpanda, Haidary Sumri, alisema madiwani wamedhamiria kutekeleza miradi yote ya maendeleo kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha.

Amesema Rais amepeleka shilingi 1,260,000,000 kwa ajili ya madarasa katika shule za msingi na sekondari, kwenye fedha za tozo kujenga kituo cha afya.

Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa, Dk. Limbu Mazoya, alizungumzia umuhimu wa tohara kwa wanaume kwa ajili ya kumkinga mwanamke na kansa ya shingo ya kizazi.

Maelezo hayo yalitokana na Diwani wa Mwamkulu, Kalipi Katani, kutoa hoja ya kulalamika kuhusu kampeni inayoendelea kutolewa ya kupunguza maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ikimtaka mwanamke asikubali kuwa na mwanaume ambaye hajafanyiwa tohara.

"Kama inapunguza maambukizi inabidi tuelimishwe sio ghafla tu, watu tumefunga ndoa mtu anakuja kusema usimkubali...hii ni hatari kwenye ndoa," alisema.

Dk. Mazoya alisema kuna ugeni ulikuja wa kamati ya Bunge nao ulisisitiza kuwa kampeni ya kumzuia mwanamke kutoshiriki tendo la ndoa na mwanaume asiye na tohara iendelee, na kwamba hiyo ni baada ya kuona kasi ya wanaume hao kujitokeza kufanyiwa tohara iko chini.

Hata hivyo, alisema kuna mpango wa kuwafanyia tohara watu wenye umri mkubwa kwa kuwatafutia wataalamu wanaoendana nao kiumri ili wafanyiwe kwa mazingira wanayoyapenda wao katika vituo vya kutolea huduma hiyo.

**Maelezo hayo yalitokana na Diwani wa Mwamkulu, Kalipi Katani, kutoa hoja ya kulalamika kuhusu kampeni inayoendelea kutolewa ya kupunguza maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ikimtaka mwanamke asikubali kuwa na mwanaume ambaye hajafanyiwa tohara.**

ama
ALHAMISI OKTOBA 28, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**USHUHUDA JIRANI...**

**Waumiza vichwa 'nini shida akili' polisi wanajiua? Ajali nazo shida!**



Ukurasa 13

Daktari bingwa: Saratani Lango la Kizazi linaepukika muhimu 'vigezo & masharti'



Ukurasa 12

**UKOMBOZI KWENYE ULEMAVU...**

**Mzazi mfugaji amwaga tabasamu na ng'ombe juu mwana kutembea**

# Zijue sababu zinazochangia shida ugonjwa akili kujirudia kila mara

**Na Dk. Raymond Mgeni**

INAELEZWA, uwekezaji mkubwa wa jamii unapaswa kuongezwa nguvu dhidi ya elimu kuhusu afya ya akili, pasipo kubagua kundi la wagonjwa wa akili.

Ni kwa sababu mtu anapopata tatizo katika afya ya akili yake, haimuathiri binafsi, bali pia wanaomzunguka. Mtu anapoathirika akili, anapoteza nafasi ya kushirikishwa katika mengi ya kijamii katika shughuli za uzalishaji mali, kwa jamii na taifa.

Ugonjwa wa akili kama yalivyo maradhi mengine yanahitaji matibabu ya kipindi kirefu na kuna wakati baadhi ya magonjwa ya akili hudumu maisha, mfano maradhi yanayoitwa 'kizofrenia nabaipola.'

Magonjwa kama wasiwasi au sonona zinapopata matibabu, huenda yatakatibika na mtu akarejea hali yake ya kawaida.

Hivyo magonjwa ya akili kujirudia hutokea kwa visa vingi vya wagonjwa wa akili na kwa namna moja hufika wakati analazwa, pale anapochanganyikiwa, mfano kupiga watu, kutisha kuua au kujiumiza mwenyewe.

Kwa kuwa ugonjwa wa akili hukaa muda mrefu kuna namna moja mtu huchoka kufuatisha au ufuasi wa dawa na hivyo kuona hakuna haja ya kuendelea na matibabu.

Hilo limesababisha mikasa mingi ya magonjwa ya akili kushindwa kutengemaa vyema, kwani yanajirudia na kuufanya ugonjwa uchelewe au kuleta ugumu wa ndugu kuendelea kumshughulikia mgonjwa, hadi kufika hatua wagonjwa wanaachwa kwa sababu ya ndugu kuchoka.

Zipo dalili za awali ambazo mgonjwa anaanza kuziona au watu wa karibu yake, ikiwamo kukosa usingizi, kupandwa na hasira isivyo kawaida, kujitenga au kukosa kuchangamana na wengine.

Ni dalili zinazoweza kutoa ishara mtu anapaswa kuanze kwenda hospitali kupatiwa matibabu la, sivyo ugonjwa utajirudia na kuleta athari kubwa zaidi.

### SABABU ZA KUJIRUDIA

Sababu ya kwanza inayochangia kujirudia kwa ugonjwa ni kuacha dawa, baada ya mgonjwa kujihisi amepona au kutafuta tiba mbadala.

Hilo linachangiwa pale dalili zilizojitokeza zikachangia mtu kulazwa baada ya dawa na kwisha.

Kuna dalili kama mtu kusikia sauti ambazo hazipo, kuvua nguo na ufahamu unapomrejea mtu huyo anagundua alichofanya si sahihi.

Pili, kuna suala la mgonjwa kuacha kudhuhuria kliniki ili kuangalia uwezekano wa kuprwa dawa za juu zaidi hasa pale tiba iliyopo isipomletea mabadiliklo, mgonjwa anaendelea kuchanganyikiwa.

Mtu anapokosa kuhudhuria kliniki kwa sababu mbalimbali ikiwemo umbali, gharama za kumwona daktari au kuhisi mgonjwa kapona kunachangia sana matatizo ya akili kujirudia. Wengi wanapokuwa wameruhusiwa baada ya kutoka wodini hushindwa kufuata taratibu za kurudi kliniki.



Dk. Raymond Mgeni, bingwa wa magonjwa ya akili Hospitali ya Rufani Mbeya. **PICHA: MAKTABA**

Tatu ni uwapo wa msongo wa mawazo kwa kipindi kirefu ni chanzo kikubwa sana kinachosababisha ugonjwa wa akili kujirudi. Mtu anapopata changamoto ngumu iwe katika kazi, uhusiano, hali ya kimaisha huchangia kuibua ugonjwa tena.

Hali ngumu za kimaisha haziepukiki ila zinaweza kudhibitiwa vizuri ili mtu asipate kuugua akili yake.

Nne ni matumizi ya vilevi au pombe kumekuwa ni sababu ya wagonjwa wengi ambao awali walipata athari za pombe au vilevi, mfano bangi kuleta uchangayikiwaji wa akili.

Hivyo vinamuathiri mtu katika kuchukua dawa zake kwa wakati au pengine siku anazokunywa pombe kusahau kabisa kunywa dawa za akili. Pili, pombe inasababisha kuzidi kuharibika kwa mfumo wa mtizamo, fikra na hivyo kuchangia zaidi mtu kupata hali ya kuchangikiwa.

Tatu, pombe inaweza kumfanya mtu kujiingiza katika vitendo hatarishi vya magonjwa, kufungwa, matumizi holela ya pesa kunakoweza zalisha matatizo mengine ya akili mfano sonona.

Nne ni Matukio yenye kuleta huzuni mfano; matukio kama misiba ambayo mgonjwa wa akili anaweza kufiwa na watu wake wa karibu huenda ni wazazi, watoto, ndugu wengine, rafiki au jamaa.

Mtu anaweza kurudiwa na ugonjwa siku chache baadaye ikiwa atashindwa kukubaliana na tukio la msiba lililojitokeza. Ndugu wa karibu ni muhimu kutoa faraja au hata mgonjwa kwenda kumwona msaikolojia ili kuepusha hali ya kujirudia kwa ugonjwa.

Kuzuia kujirudia rudia kwa ugonjwa ni muhimu kuzingatia haya ambapo mgonjwa mwenyewe anaweza kushindwa ila wanaomzunguka wakahusika kumsaidia hilo.

Ufuasi wa dawa unaweza kusaidiwa na ndugu kukumbusha mgonjwa kunywa dawa zake, pia kukumbusha kurejea tarehe ya kliniki, kumzuia katika kurejea katika unywaji wa pombe, vilevi, kusaidiwa kudhibiti athari za msongo wa mawazo.

Niseme, kuishi vizuri na mgonjwa kwa kuepuka unyanyapaa, lugha za kudhalilisha na kunyima haki za mgonjwa wa akili.

***• Anapatikana kwa simu: +255 676 559 211 ua barua pepe: raymondpoet@yahoo.com katika Hospitali ya Kanda Rufani Mbeya.***

AFYA

UKOMBOZI KWENYE ULEMAVU...

# Mzazi mfugaji amwaga tabasamu na ng'ombe juu mwanawe kutembea

**Na Christina Haule,** Morogoro

• Alikata tamaa, Padre akajibu 'yawezekana'

ILIKUWA hoihoi ya aina yake kuibuliwa pale mtoto aliyefanikishiwa nafuu kimaisha kutokana na ulemavu, hata mhusika mkuu Mkurugenzi wa Kituo cha Kulelea Watoto Wenye Ulemavu wa Viungo na Akili (Amani Center) mkoani Morogoro, Padre Beatus Sewando, akajikuta anazawadiwa ng'ombe.

Huyo ni kati ya watoto 12 wenye ulemavu  kutoka kundi la 84 waliokwishapelewa katika Hospitali ya Rufani Muhimbili, kitengo cha CCBRT, wakifanyiwa upasuaji na wanaelezwa wanaendelea vizuri, huku wengine wakibaki kwenye matawi ya hospitali ya CCBRT wakipatiwa matibabu, mazoezi na elimu ya msingi.

Ilikuwa furaha ya mtoto mmojawapo kutoka jamii ya wafugaji, mzazi wake alipoona mtoto huyo kapona baada ya kusumbuliwa na ulemavu kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuzaliwa.

Padre Sewando anavitaja vijiji wanakotoka watoto hao wanaoibuliwa ni Mandela mkoani Pwani, Matombo na Kiroka (Morogoro Vijijini), Chakwale na Magubike (Gairo), Dakawa na Lumbiji wilayani Kilosa.

Anasema katika kipindi cha mwaka jana hadi huu, waliibua watoto hao kwenye vijiji jumla yao 84 waliofichwa majumbani, katika uwiano 17 waliibuliwa mwaka jana na 67 mwaka huu.

### WALIVYOANZA KAZI

Padre Sewando anasema, baada ya elimu ya kuwatunza na maelekezo kutolewa na Amani Centre walipotembelea vijiji hivyo, kikiwamo Twatwatwa kilichoko tarafa ya Kimamba wilayani Kilosa, baadhi ya wazazi wa watoto wenye ulemavu walianza kuelewa na kujitokeza.

Anasema, baada ya kufanikiwa kuwapata wazazi wawili akiwamo Parisiato Lamaray (47), baba wa mtoto asiyeweza kuinuka kitandani aliende naye hadi kituoni kufuata matibabu na mazoezi.

Padre Sewando anasimulia, baada ya kumuelimisha Lamaray mtoto wake Yona Parisiato angeweza kupona, alikubali na kumruhusu kuondoka naye kwa ahadi kama angepona angempa ng'ombe mmoja. Anafafaua kuwa, baada ya matibabu na mazoezi kwa miezi mitatu, mtoto alianza kusimama na hatimaye kutembea, kitendo kilichomfanya mzazi kutimiza ahadi yake kwa furaha iliyopitiliza.

Mkuu huyo wa kituo cha Amani, anasema katika mizunguko yake amegundua kuwapo wenye ulemavu katika jamii za wafugaji wasiopatiwa huduma za kitabibu, huku akipata taarifa huduma pekee zinazotoelewa kwa watoto ni chakula.



Baba mzazi Parisiato Lamaray, amembeba mwanawe Yona, kwa furaha, baada ya Amani Centre kumtembelea kijijini Twatwatwa, wilayani Kilosa. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

> **Mimi sikukata tamaa, mwanangu wa pili alizaliwa akiwa amelegea viungo vyote na siku zilivyokuwa zinazidi kusonga mbele ndipo mwanangu alipoonyesha kulegea zaidi.**

Imegundulika kuwapo falsafa inayotoa uzito kwa ndama akiwa na thamani ya pesa kutokana na tabia ya kuhama na wamekuwa wakiwaacha watoto wenye ulemavu kwenye maboma, wakiwaona ni mzigo.

Hivyo Padre Sewando anaitaka jamii kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu ndani bali wawatoe nje na kupata huduma zinazostaili na kwamba, kumficha ndani mtoto ni kitendo kibaya kinachodhuru haki zake za msingi, ikiwamo elimu, kupendwa, kuthaminiwa, kupata matibabu na afya bora.

Anaeleza watoto hao walioibuliwa, wapo wanaoendelea na matibabu na mazoezi kwenye Kituo cha Amani Chamwino, wengine wanasoma elimu ya awali mahali hapo.

Pia, wapo wanaosoma katika shule ya elimu maalum iliyopo kwenye tawi la Amani iliyopo Mvomero, hali kadhalika wanaopatiwa elimu ya maisha katika tawi la Amani Mikese.

### KUKOSA LISHE

Padre Sewando anafafanua katika kuibua huko wapo watoto wanaodhaaniwa walemavu, hukutwa kinyume chao ni shida ya udhaifu kiafya unaotokana na kukosa lishe sahihi.

Katika hili, anafafanua kwamba watoto wanapokuwa wadogo wanapaswa kula vyakula vilivyokamilika, hata kumekuwapo mabadiliko kwa jamii ya kifugaji, ambao wamekuwa wakila nyama na maziwa pekee.

Anafafanua, kwa sasa wanatumia pia ugali kidogo, matunda na mboga za majani jambo ambalo inayowajengea mwili na hawadhoofiki, wanapata mahitaji muhimu kiafya, ikiwamo madini na vitamini.

"Nawashauri kinamama kwa 'wababa' wa Kimasai mjenge tabia ya kutengeneza bustani ndogo nyumbani na kupanda mboga za majani mtazozimwagilia maji kila siku. Zitawasaidia kupata mboga na kuboresha afya zenu" anasema Padre Sewando.

### WAZAZI WANENA LAO

Mzazi Parisiato anayetoa ng'ombe kwa Mkurugenzi wa Kituo cha Amani baada ya mwanae kusimama na kutembea, anafafanua ameamua kumpa ng'ombe mkuu huyo kwa kutimiza wajibu wake kwa mtoto kufikia kupona, kwani binafsi alishakata tamaa.

Parisiato anasema, awali mwanae Yona Parisiato alikuwa na mwili mlegevu, asiyemudu ama kujisogeza au kufanya lolote tangu umri mtoto mchanga, jambo lililompa shaka na mkewe wakihisi ulemavu tangu kuzaliwa.

Anasema, wamehangaikia matibabu hayo pasipo mafanikio, hadi ulipotokea uongozi wa kituo cha Amani Centre waliomchukua mtoto kwa mazoezi na tiba, sasa matunda yanaonekana akitembea.

Parisiato anasema, baada ya mwanae kupona binafsi amekuwa balozi mzuri wa kuhamasisha wanavijiji wenzake hadi kwenye kata, kuwatoa watoto wenye ulemavu kwani ipo tiba sahihi na mazoezi kwa ajili ya kasoro hizo.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, kupona kwa mtoto wake kumeamsha ari ya kitongoji na kijiji kizima kuamua kupeleka watoto wenye ulemavu kupatiwa matibabu na mazoezi.

"Naishukuru Amani Centre imenitia sana moyo kwa kuona mwanangu anasimama mwenyewe bila kushikwa kabisa, sijui wanatumia dawa gani, kweli namshukuru Mungu," anasema

Mama mzazi wa mtoto Yona, Agnes Ngale (24), anasema wamekuwa wakiwabeba watoto wenye ulemavu na kuhama nao pale inapobidi na sio kuwatelekeza kama ilivyokuwa zamani.

Agnes anawashauri wanawake wenzake wenye watoto wenye ulemavu, wasikate tamaa kuwahudumia watoto wao bali, wawapeleke kwenye vituo vya kufanya mazoezi wakapate tiba sahihi, ili nao watembee.

"Mimi sikukata tamaa, mwanangu wa pili alizaliwa akiwa amelegea viungo vyote na siku zilivyokuwa zinazidi kusonga mbele ndipo mwanangu alipoonyesha kulegea zaidi.

"Tukaanza utaratibu wa kumpatia matibabu na sasa ana miaka mitatu ameweza kusimama vizuri, tunasubiri asogee kukua, tumuangalie kiakili, aanze shule" anasema mama huyo.

### BABU MFUGAJI KIJIJINI

Mzee wa wafugaji, Farais Makala (70), mkazi wa kijiji cha Twatwatwa kata ya Kimamba wilayani Kilosa, anakana jamii hiyo kuwatelekeza kwenye maboma watoto wao walemavu hadi kusababisha vifo, kwani zamani hawakupata watoto wenye ulemavu, labda wenye ulemavu wa mguu mmoja pekee.

Anajitetea kwamba suala la wafugaji kuhama na kuacha watoto wenye ulemavu kwenye maboma wakati wakihama kwa madai 'ni mzigo usio na faida zaidi ya ndama' ni misemo isiyo na ukweli ndani yake.

Mzee Makala anasema wamekuwa wakipata watoto wenye ulemavu zaidi hivi sasa, wakiwamo wenye vichwa vikubwa, wasiosikia na wasioona, huku wakijitihadi kuwatafutia matibabu na walipogundua Kituo cha Amani mkombozi wa watoto wao, wanapatumia.

AFYA

# Daktari bingwa: Saratani Lango la Kizazi linaepukika muhimu 'vigezo & masharti'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

- Kujikagua, mwenendo wa mapenzi…
- Atahadharisha ishara bado si salama

RIPOTI ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2010, inaonyesha hadi wakati huo nchini kuna wastani wa wanawake 6,241 wanaougua saratani ya shingo ya kizazi kila mwaka, 4,355 kati yao wamefariki kwa ugonjwa huo.

Aidha, takwimu za dunia zinaonyesha saratani hiyo iko juu katika kusababisha vifo vya wanawake wengi duniani, ikikadiriwa asilimia 85 ya vifo hivyo vinatokea katika nchi zinazoendelea.

Daktari Harryjustin Mwambe, bingwa wa tiba ya magonjwa ya kinamama na afya ya uzazi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma, anasema saratani hiyo ndio iko juu kwa wanawake nchini walio na umri kati ya vijana wa miaka 15 hadi kwa watu wazima wenye umri miaka 44.

"Tanzania ina wanawake milioni 10.97 walio na umri wa miaka 15 na kuendelea, ambao wako kwenye hatari kubwa ya kupata saratani hii. Kwa Afrika Mashariki, asilimia 33.6 ya wanawake wote wanasadikiwa kuwa na virusi aina ya 'Human Papilloma Virus' (HPV) ambavyo ndio visababishi vikuu vya ugonjwa huu," anafafanua.



Sehemu ya Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma. **PICHA: MAKTABA.**

**IKOJE HIYO?**

Dk. Mwambe anaieleza ni mabadiliko hasi (yasiyo ya kawaida) ya chembechembe hai zilizopo kwenye shingo ya kizazi, ambayo mara nyingi saratani inapoanza huwa haionyeshi dalili yoyote, hivyo mgonjwa hawezi kuchukua hatua yoyote kukabiliana na tatizo hilo kwa wakati huu.

"Kwa kiasi kikubwa saratani hii husababishwa na maambukizi ya muda mrefu (persistence infection) ya virusi viitwavyo 'human papilloma' ambayo huenezwa kwa njia ya kujamiiana.

"Kawaida mwili una uwezo wa kudhibiti maambukizi haya yaingiapo mwilini, lakini yasipodhibitiwa kikamilifu na kuwapo mwilini kwa muda mrefu, husababisha ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi," anaeleza Dk. Mwambe.

Anasema, saratani hiyo inapoanza huwa ni vigumu sana kugundulika, kwa sababu haionyeshi dalili, hivyo inagundulika ikiwa imefikia hatua mbaya zaidi.

"Dalili kama kutokwa na majimaji au maumivu wakati wa tendo la ndoa, seli za saratani ya shingo ya kizazi hukua taratibu na huchukua miaka mingi kwa seli za kawaida kubadilika kuwa saratani. Ndio maana inashauriwa kufanya uchunguzi mara kwa mara, ili kugundua mapema,"anasema.

**CHANZO NINI?**

Dk. Mwambe anasema, aina zote za saratani ya shingo la kizazi huanza na maambukizi ya muda mrefu ya moja ya virusi viliyotajwa vya 'human pappiloma,' akiwa na ufafanuzi wa kitalaamu kwamba:

> **Upasuaji hufanya kwa kuondoa nyumba ya uzazi na matezi ambayo yapo kwenye nyonga na kuondoa sehemu ya juu ya uke (Radical Hysterrectomy).**

"Utafiti unaonyesha kwamba watu wengi wanaambukizwa virusi hivi katika muda fulani wa maisha yao. Maambukizi haya mara nyingi hupona yenyewe, kwa kutumia kinga ya mwili iliyopo."

Hata hivyo, anasema kwa baadhi ya wanawake maambukizi hayo huendelea kudumu kwa muda mrefu na kuleta mabadiliko kwenye chembe hai za shingo la kizazi.

Namna ya kugundua uwapo wake, Dk, Mwambe anasema mtu huchunguzwa kwa mujibu wa miongozo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Hata hivyo, kuanza vitendo vya ngono katika umri mdogo na uhusiano wa kimwili na zaidi ya mwanamume, zimo katika visababishi vinavyoongoza kwenye maradhi hayo.

**NINI KIFANYIKE?**

Dk. Mwambe anasema, suala la matumizi ya chanjo ya saratani ya shingo la kizazi kwa watoto wenye umri kati ya miaka tisa na 14 na utekelezaji programu iliyoanzishwa na wizara inayohusika na afya, kwa kutoa chanjo kwa wasichana wa shule za msingi walioko kati umri huo, kuwanusuru na janga hilo .

"Chanjo hii huzuia maambukizi ya saratani ya shingo la kizazi kutoka 'high risk- HPV' (walio ha-



Daktari Harryjustin Mwambe, bingwa wa tiba ya kinamama katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma. **PICHA: AGUSTA NJOJI**

tarini zaidi), pia kufanya uchunguzi wa saratani ya shingo la kizazi na matibabu kwa saratani ambayo iko katika hatua za awali kabisa,"anasema.

Mtaalamu huyo ana ushauri kwa kinamama kwamba, waanze uchunguzi wa afya zao kuanzia umri miaka 30 hadi ukomo wa hedhi.

"Kipimo kikiwa hasi (negative) uchunguzi utafanyika kila baada ya miaka mitatu na endapo kimo kitakua chanja (positive) mgonjwa atapewa matibabu ya krayotherapia (cryotherapy) na atarudi kila baada ya mwaka mmoja kwa uchunguzi," anasema.

Pia, anahimiza katika elimu ya afya katika maeneo kadha ikiwamo: Kuepuka ngono kwa wasichana walio kwenye umri mdogo; kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu; kubadilisha mwenendo wa maisha kama kuepuka matumizi ya pombe na sigara kwa kadri inavyowezekana.

**MATIBABU YALIVYO**

Mtaalamu huyo anasema saratani ya shingo la kizazi inatibika endapo itagunduliwa mapema na iko kwenye hatua za awali.

"Hutegemea mambo mbalimbali ikiwamo hatua ya saratani iliyofikiwa wakati wa uchunguzi. Kwa kawaida ikiwa katika hatua za awali kabisa matibabu ya kryotherapia yanafanyika, sambamba na mengine kwa wakati mmoja," anaeleza

Dk. Mwambe anaorodhesha mbinu hizo, ni pamoja na upasuaji, tiba ya mionzi (radiotherapy), matumizi ya dawa (chemotherapy), na 'tagerted therapy' kwa saratani anayoisema tayari inakuwa imeshasambaa.

Anaeleza upasuaji huo hufanywa kwa kuondoa sehemu iliyoathiriwa na saratani, hasa iliyoko kwenye hatua za awali, daktari akifafanua:

"Upasuaji hufanya kwa kuondoa nyumba ya uzazi na matezi ambayo yapo kwenye nyonga na kuondoa sehemu ya juu ya uke (Radical Hysterrectomy). Aina hii ya upasuaji hufanywa kwa wanawake ambao tayari wameshamaliza kuzaa."

Anaorodhesha aina nyinginezo za upasuaji wa kuondoa sehemu ya ndani ya shingo la kizazi ambako uvimbe huanzia (cone biopsy) na kuondoa sehemu ya juu ya uke na shingo la kizazi.

Pia kuna tiba ya mionzi, ambayo Dk. Mwambe anaieleza: "Ni tiba inayotumika kwa wagonjwa walio wengi. Hutolewa kwa mionzi ya nje na mionzi ya ndani, kama tiba ya mionzi imechaguliwa kama njia kuu ya saratani ya shingo la kizazi basi 'chemotherapy' inatumika kama njia saidizi."

Daktari huiyo anasema ni matibabu ya kutumia dawa na mara nyingi hutumika sambamba na tiba ya mionzi katika hatua za saratani ya shingo la kizazi.

"Tiba maalum ya seli ni tiba inayohusisha matumizi ya dawa maalumu, ambayo imetengenezwa kwa ajili ya kusimamisha shughuli za seli zinazochangia ukuaji wa seli za kansa na hutolewa kwa saratani iliyofikia hatua ya juu," anasema.

Tabibu bingwa, Mwambe, anadokeza kuwa ni saratani inayoepukika na inatibika pale inapogundulika mapema, hivyo rai yake ni kufanyike uchunguzi wa mapema na kila mara, kwa kuzingatia miongozo iliyoko kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na watoto.

AFYA

USHUHUDA JIRANI...

# Waumiza vichwa 'nini shida akili' polisi wanajiua? Ajali nazo shida!

**Na Mwandishi Wetu**




Polisi wa Usalama Barabarani, wakiwajibika nchini Kenya katika mtazamo tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

INAWEZA kuwa taarifa ya kusikitisha, ikiwamo za takwimu kutoka Shirika Huru la Kutetea Haki za Waathiriwa Kisheria na Kimatibabu la (IMLU) nchini Kenya, zinaonyesha kuwapo maofisa 20 wa polisi ama wameuawa au walijiua tangu, Januari mwaka huu hadi mwezi ulioisha.

Shirika hilo linasema vifo hivyo vimetokana na matatizo ya afya ya akili, hali inayoibua shaka miongoni mwa walinda usalama hao.

Ripoti ya shirika la IMLU, inasema mikasa ya maofisa wa Polisi ama kuuana au kujiua, inazidi kushuhudiwa katika pembe mbalimbali za Kenya, ikielezwa baadhi ya magumu ni zao la maudhui ya kazi zao, huku nyingine zikichangiwa na matatizo ya kawaida kimaisha.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa maofisa hao wanahitajika kudumisha sheria na utangamano katika mazingira magumu, hivyo kuhatarisha maisha yao, kila siku wanapoamka.

Caroline Tunen, Ofisa Mipango wa Shirika la IMLU anafafanua: "Maofisa 21 wamejiua ama wameua wenzao, kutoka mwezi Januari. Hiyo ni idadi kubwa na tunajua kwa idara ya Polisi imeweka mikakati ya kuangazia suala hilo ambalo ni la dharura."

Mkasa wa kuuwa Konstebo wa polisi mwenye umri miaka 28, tendo lialodaiwa kutokea kwa mpenzi wake mwezi Julai, ni ukumbusho anaoutaja Caroline, ni namna afya ya akili inapaswa kuchukuliwa kwa unyeti wake.

Pia, kuna mkasa wa askari kuua mtu alipokuwa akitoroka mamlaka. Baadaye inadaiwa alijitoa uhai, kwa kujipiga risasi nyumbani kwake.

Ripoti ya IMLU ina mtazamo: "Mchango mkubwa kwa hali hii unatokona na mazingira ya utendaji kazi wa polisi, hali kadhalika masuala ya kijamii, ambayo huwashinikiza kutenda visa vya kutisha, japokuwa wao ndio walinda usalama."

IMLU inataja baadhi ya viashiria vinavyochangia msongo wa mawazo, kujitoa uhai na hata kuuana miongoni askari polisi wa Kenya.

Gacheke Gachuhi, ni mwanaharakati wa kutetea haki za binadamu nchini Kenya, analaani mauaji ya kiholela anayodaia kutekelezwa na askari polisi, akitaja yanatokea kila siku na yanawadhuru akili zao.

> **Kumekuwapo malalamiko mengi kwamba kuna ongezeko la ajali, lakini tunajiuliza idadi ya magari yanayoongezeka barabarani kila mwaka? Barabara haziongezeki.**



Mnamo Juni mwaka huu, Wizara ya Afya nchini Kenya ilizindua Mpango wa Utekelezaji wa Afya ya Akili Kenya ya miaka mitano kuanzia mwaka ujao, 2022.

Aidha kuna muswada wa marekebisho wa Afya ya Akili katika Bunge la Seneti kukiwapo wito wa pamoja kutoka kila pembe ukinuia kutangaza tatizo hilo kuwa janga la taifa.

**MIKASA AJALI**

Utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama nchini Kenya NTSA unaonyesha zaidi ya watu 3,000 wamekufa nchini humo, kutokana na ajali za barabarani, kuanzia mwaka 2021

Ripoti inabainisha kiwango ni cha juu nchini Kenya maradufu, kwani mwaka uliotangulia ni wastani wa chini zaidi.

Utafiti huo mpya umechunguza ajali za barabarani tangu Januari 2021 hadi mwezi Septemba na kuonyesha Wakenya 3200 walikufa ndani ya kipindi cha miezi tisa pekee.

Ripoti hiyo inasema, miongoni mwa walioaga dunia mwaka huu: Watu 1,100 wanatembea kwa miguu; madereva 300; abiria 318; waendesha bodaboda 890; na waendeshaji baiskeli 61.

Sababu kuu katika ajali hizo zinatajawa ni madereva kutozingatia sheria za barabarani mwendo kasi kupita kiwango, ulevi wa madereva na waendesha pikipiki na baiskeli.

Naibu Mkuu wa Polisi wa Kenya, Edward Mbugua, ananyoshea kidole cha lawama ukosefu wa kuongezeka kwa miundo mbinu.

"Kumekuwapo malalamiko mengi kwamba kuna ongezeko la ajali, lakini tunajiuliza idadi ya magari yanayoongezeka barabarani kila mwaka? Barabara haziongezeki," anatamka Kamanda Edward.

Felix Ochieng, mchambuzi wa masuala ya kijamii, anatoa mtazamo wake kuwapo mikasa 2,820 ya ajali kwa sasa, dhidi ya mikasa 2,200 mwaka uliopita.

Ni jambo linalowaumiza vichwa maofisa wakuu wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama nchini Kenya, waliokutana na uongozi wa polisi kuangazia suala hilo na miongoni mwa yanayojitokeza mapema ni madereva kutozingatia sheria za barabarani.

Walikubaliana kuongeza kampeni kudhibiti vyanzo vya ajali vinavyosababisha maafa, pia kuwaachia wengi majeraha.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Chama cha Usalama Barabarani, David Kiarie, analaumu NTSA kwa uzembe ambao umechangia ongezeko la ajali barabarani.

Asasi ya NTSA inasema kuwa itashirikiana na serikali za majimbo kupitia kamati za usafiri na usalama kutafuta mbinu za kupunguza ajali za barabarani, mkakatio utakaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

***Kwa mujibu wa DW.***



## Wahimiza sheria ya bima afya kwa wote

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa sheria ya bima ya afya kwa wote kwa itakuwa mwarobaini wa kusaidia wananchi kupata huduma za afya kwa uhakika.

Rai hiyo ilitolewa juzi kwenye mkutano wa kamati za dini na wadau wa afya jijini hapa.

Katika mkutano huo, viongozi hao wa kamati za dini walisema kupitisha kwa sheria hiyo kutakuwa mkombozi kwa Watanzania ambao wanakosa huduma za afya kutokana na kukosa fedha na wale wenye uchumi mdogo.

Mwenyekiti wa Baraza la Maaskofu Kanisa la Menonite, Askofu Nelson Kisare, alisema utafiti ulifanyika walipata majibu na walitengeneza kitabu na wanatumia utafiti kushawishi serikali kuwa na sheria bora ambayo itakuwa inatoa haki kwa kila mwenye uhitaji.

"Kwa kweli sisi viongozi wa dini tunatoa shukrani zetu kwa serikali. Tumesikia katika hotuba Rais akizungumzia Wizara ya Fedha na Mipango ilete fedha ili muswada huo upitishwe. Nichukue nafasi hii kuipongeza serikali kwa juhudi hizi wanazofanya," alisema.

Askofu Kisare alisema lengo la mkutano ni nini kifanyike ili kupata sheria ambayo itasaidia watu wenye kipato cha chini.

"Sasa tumekutana nini kifanyike ili tuwe na nia moja lengo moja tupime kwa pamoja ili tupate sheria ambayo itatusaidia matumaini yetu ni kwamba tutajaliada kwa amani na upendo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Khamis Mataka, alisema katika jamii kwa sasa hali ni mbaya, hivyo inahitajika sheria ya bima kwa afya ili kuwakomboa.

Mratibu wa Kamati ya Amani Taifa, Edmund Matotay, alisema wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2020 vyama mbalimbali viliinadi sera ya bima ya afya kwa wote na vilidai vikichukua nchi bima ya afya kwa wote itaanza kutumika.

Mratibu huyo alisema baada ya uchaguzi Rais (Hayati Dk. John Magufuli) alitamka serikali ipeleke mchakato wa muswada wa bima ya afya kwa wote.

# LAAC yaibua madeni bil. 1.4/- Halmashauri ya Mji Makambako

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imeshtushwa na uwapo wa deni kubwa katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe lenye thamani ya Sh. bilioni 1.4.

Deni hilo linatokana na na madai mbalimbali zikiwamo stahiki za watumishi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kufanya mahojiano na halmashauri hiyo kuhusu hoja za ukaguzi za mwaka 2019/20, Makamu Mwenyekiti wa LAAC, Selemani Zedi, alisema wamebaini kuwa halmashauri hiyo ina deni kubwa na kati ya fedha hizo, Sh. milioni 167 inadaiwa na wafanyabiashara mbalimbali.

"Pia kuna deni la Sh. milioni 247 inadaiwa na watu ambao ilipaswa kuwalipa fidia ya viwanja vyao, lakini kuna karibu Sh. bilioni moja ambayo inadaiwa na watumishi mbalimbali wakiwamo walimu, likizo za mishahara iliyopunjwa, iliyochelewa na watu ambao hawajapandishwa madaraja," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Zedi alisema kamati hiyo imeagiza halmashauri kutengeneza mpango maalum wa kulipa madeni hayo.

"Kwa sababu namna tulivyowahoji na kujieleza, ilionekana Halmashauri ya Makambako haina mpango wowote wa kuyalipa haya madeni na unapokuwa na madeni, lazima uwe na mpango wa kulipa. Yale yanayopaswa kulipwa kwa fedha za ndani mpango ukoje mmetenga kila robo mlipaje na yale yanayolipwa kutoka serikali kuu mpango ukoje.

"Mnafuatiliaje? Wanalipaje? Tulibaini kuwa halmashauri haina mpango wowote wa kulipa madeni," alisema.

Aliagiza kabla ya mwisho wa Desemba, mwaka huu, mpango huo uwe tayari umekamilika na nakala ipelekwe kwa Mkaguzi wa Mkoa na kamati ipate nakala.

Awali, alifafanua kuwa kuna dosari zilibainika kwenye hesabu hizo zikiwamo katika eneo la ununuzi na mikataba.

"Taarifa ya mkaguzi imebaini kulikuwa na ukiukwaji wa sheria ya ununuzi katika maeneo kadhaa. Utoaji wa zabuni katika maeneo kadhaa ulikuwa hauzingatii sheria ya ununuzi kwa maana kwamba hakukuwa na ushindani katika utoaji wa zabuni," alisema.

Alisema katika mikataba, ukaguzi umebaini kulikuwa na baadhi ya mikataba inafungwa na iliyokuwa inaingiwa kati ya halmashauri na mawakala wa kukusanya mapato.

"Mikataba hiyo ilikuwa haisainiwi (haitiwi saini) na watu ambao walikuwa na nguvu za kutia saini mikataba baadhi ya mawakala walikuwa hawatimizi makubaliano. Kazi ya wakala ni kukusanya mapato na kuyaleta halmashauri," alisema.

Aliongeza kuwa mawakala wanne walibainika kuwa walikuwa hawafikii malengo ya ukusanyaji wa mapato na kuyapeleka katika halmashauri kwa sababu mikataba yao na halmashauri ilikuwa haijatiwa saini kisheria.

"Hakuna tena nafasi ya kuwafikisha katika vyombo vya sheria au kuwachukulia hatua kwa sababu mkataba wenyewe haukuwa umefungwa kihalali kwa hiyo eneo la kwanza," alisema.

Kutokana na kasoro hizo, alisema kamati imemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe kupitia kitengo cha usimamizi kutengeneza mpango maalum ili mji wa Makambako uwe na uwezo katika maeneo hayo ya usimamizi wa mikataba na utoaji wa zabuni.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Fx Heding Victory, Victor Maeda (kulia), akimkabidhi Joseph Msandawe mtaji wa kuanzia wa dola za kimarekani 200, baada ya mafunzo ya kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri kwa njia ya ubadilishaji fedha za kigeni kwa njia ya simu, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mchungaji ahimiza utamaduni wa kusoma vitabu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kutumia muda wao kusoma vitabu vinavyowaelimisha na kuongeza maarifa badala ya kutumia muda mwingi kuangalia picha kwenye mitandao ya simu.

Katibu Mkuu wa Makanisa ya Pentecostal Holliness Assiciotion Mission Tanzania, Mchungaji Ally Mwasunga, alitoa ushauri huo jana katika hafla ya kuzindua kitabu chake cha 'Umuhimu wa Moto Katika Maisha ya Kikristo'.

Alisema bado kuna mwitikio mdogo kwa Watanzania hususani linapokuja suala la kusoma vitabu.

Mwasunga alisema hali hiyo inawakosesha watu kupata maarifa ambayo yamo kwenye vitabu vilivyoandikwa na watunzi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Watanzania tunatakiwa kuwa na tabia ya kujisomea vitabu mbalimbali vinavyoandikwa na watunzi ili kujifunza na kutambua mahitaji mbalimbali yanayoweza kutusaidia wenyewe pamoja na taifa," alisema.

Pia alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya Watanzania kutokuwa na muda wa kusoma vitabu na wengi hutumia wakati wao kwa shughuli ambazo hazina msingi tofauti kama wangetumia kusoma vitabu.

Kadhalika, aliwaomba wazazi na walezi kuwahimiza watoto wao kupenda kusoma vitabu vyenye maadili mema ya kimwili na kiroho ili kuwa watunzi wazuri wa vitabu vitakavyoelimisha jamii kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema wazazi pamoja na walezi hawana budi kuwajengea mazoea watoto wao kusoma vitabu mbalimbali na kwamba kwa kufanya hivyo, watakuwa wamewawezesha pia kutumia muda huo kuepuka kuangalia vipindi vya runinga ambavyo havina tija kwao na masomo yao.

"Wakiwahamasisha kupenda kusoma vitabu mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiroho, taifa linaweza kuwapata wasomi ambao watakuwa na uwelewa mpana tofauti na ilivyo sasa kwa vijana wengi kuangalia picha zisizokuwa na tija," alisema.

International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

# INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK (TANZANIA) LIMITED

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.09.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 30.09.2021 | 30.06.2021 |
| A. | ***MALI*** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 983 | 1,080 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 5,210 | 15,177 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 8,867 | 7,278 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,988 | 4,299 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 46 | 34 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 34,689 | 34,879 |
| 12 | Mali Nyingine | 11,061 | 9,853 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,112 | 1,149 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **68,955** | **73,748** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,000 | 0 |
| 18 | Amana za Wateja | 35,339 | 44,643 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 162 | 162 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 3 | 73 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 749 | 1,198 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 62 | 62 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,368 | 3,051 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | ***JUMLA YA DHIMA*** | **42,682** | **49,189** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **26,273** | **24,559** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,709 | 29,975 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 14,051 | 7,639 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (17,951) | (11,539) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (2,537) | (1,516) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **26,273** | **24,559** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 736 | 1,176 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 23,053 | 21,021 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 3,287 | 2,837 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38.10% | 33.30% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 54.52% | 50.72% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 109.83% | 92.49% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 50.31% | 55.22% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 73.30% | 62.99% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -14.07% | 32.74% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -6.50% | 17.89% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.09.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.09.2021 | 30.09.2020 | 30.09.2021 | 30.09.2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,205 | 1,073 | 3,298 | 4,287 |
| 2 | Gharama za Riba | 412 | 547 | 1,263 | 2,048 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***793*** | ***526*** | ***2,035*** | ***2,239*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 172 | - | 173 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 450 | 859 | 788 | 1,520 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **225** | **282** | **491** | **928** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 33 | 14 | 52 | 96 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 30 | 45 | 88 | 143 |
| | 6.3 Gawio | - | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 163 | 223 | 351 | 689 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,406** | **1,357** | **4,090** | **4,106** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 579 | 563 | 1,749 | 1,744 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 54 | 16 | 180 | 82 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 772 | 778 | 2,160 | 2,280 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,009)** | **(1,408)** | **(2,525)** | **(2,458)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 12 | - | 12 | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,021)** | **(1,408)** | **(2,537)** | **(2,458)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,021)** | **(1,408)** | **(2,537)** | **(2,458)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 57 | 59 | 57 | 59 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (51) | (70) | (127) | (123) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (51) | (70) | (127) | (123) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 5 | 4 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -5.74% | -7.54% | -4.97% | -6.59% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -16.11% | -27.32% | -13.16% | -15.58% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 98.28% | 100.16% | 107.94% | 78.73% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 6.56% | 3.50% | 5.35% | 5.02% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 30.09.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.09.2021 | 30.06.2021 | 30.09.2021 | 30.09.2020 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,009) | (1,026) | (2,525) | (2,479) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 683 | 404 | 1,151 | 1,618 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (431) | 1,097 | 82 | 4,523 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (6,304) | 11,051 | 968 | (9,903) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (202) | 168 | (265) | 2,020 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,208) | (380) | (1,306) | (3,541) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (12) | - | (12) | - |
| | -SMR | (385) | 56 | (62) | 1,203 |
| | - Mengineyo | - | (36) | (36) | 431 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(8,868)*** | ***11,335*** | ***(2,004)*** | ***(6,127)*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (24) | (90) | (869) | (61) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | | - | |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (1,589) | (2,045) | 1,150 | (10,129) |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(1,613)** | **(2,135)** | **281** | **(10,190)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 2,734 | 1,035 | 3,769 | 4,727 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **2,734** | **1,035** | **3,769** | **4,727** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(7,747)** | **10,235** | **2,046** | **(11,591)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 18,546 | 8,311 | 8,753 | 16,677 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **10,799** | **18,546** | **10,799** | **5,086** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Saini:

**VILLY VELLAYAPPAN**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 26 Oktoba 2021

**GEORGE MSAMBAZI**
Mkuu wa Fedha
Tarehe: 26 Oktoba 2021

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 26 Oktoba 2021

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

Saini:

**VISWANATHAN SUNDARAM**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 Oktoba 2021

**HASHIMAH BINTI ISMAIL**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 26 Oktoba 2021

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.09.2021

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **28,940** | | **(11,320)** | **7,455** | | - | **25,076** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (36) | - | | | **(36)** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (2,537) | | | | **(2,537)** |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | | | | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 3,769 | | (6,596) | 6,596 | | | 3,769 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.09.2021** | **32,709** | - | **(20,489)** | **14,051** | - | - | **26,273** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **20,025** | | **(4,086)** | **4,140** | | - | **20,079** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (109) | | | | (109) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (3,809) | | | | (3,809) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (3,315) | 3,315 | | | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 8,915 | | | | | | 8,915 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2020** | **28,940** | | **(11,320)** | **7,455** | | - | **25,076** |





# Watu waanguka wakivuna karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU watatu wamefariki dunia baada ya kuanguka katika mikarafuu na wengine 78 wamepata majereha mbalimbali katika matukio hayo tangu kuanza kwa msimu wa karafuu mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, Maisara mjini Zanzibar, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC), Said Seif Mzee, alisema watu hao ni 78, mmoja ni kutoka Unguja na 77 Kisiwani Pemba. Alisema wameanguka wakiwa katika uchumaji wa karafuu katika msimu ulioanza Julai hadi Oktoba, mwaka huu.

Said alisema watu hao walioanguka katika mikarafuu wanaume ni 56 na wanawake ni 22 na watatu waliofariki dunia wote ni wanaume. Kutokana na ajali hizo, ZSTC imekata bima kwa ajili ya kuwalipa fidia majeruhi hao na kwa mwaka huu wameshalipa Sh. milioni 174.6.

Alisema mwaka huu msimu wa karafuu umeanza mapema na ni mkubwa ikilinganishwa na misimu mingine, hivyo wanatarajia kununua tani nyingi zaidi kuliko mwaka jana.

"Msimu wa mwaka huu tumeanza Julai na msimu huu ni mkubwa ambao unaweza kufanana na msimu wa mwaka 2017/18 ambao tulipata tani 8,572, hivyo tunatarajia kufikia tani hizo 8,572," alisema.

Alisema vituo vikubwa vya uuzaji wa karafuu ni Wete, Mkoani na Chakechake Pemba lakini mahitaji yanapozidi shirika hilo hufungua vituo vingine.

Mkurugenzi huyo alisema ununuzi wa karafuu kwa mwaka huu ni mzuri na wakulima wamelipwa bei ambayo serikali imetangaza ambayo ni Sh. 14,000 kwa daraja la kwanza, Sh. 13,000 kwa daraja la pili na Sh. 12,000 kwa daraja la tatu.

Hata hivyo, alsiema kumekuwa na malalamiko kuwa wakulima hawapati daraja la kwanza la karafuu jambo ambalo si la kweli kwa sababu shirika limeshanunua karafuu za daraja la kwanza kutoka kwa wakulima.

Ili mkulima kupata daraja la kwanza kunahitaji kazi za ziada tokea karafuu zinapochumwa, zinaposafirishwa, zinapoanikwa na kufuata vigezo vilivyowekwa ikiwamo kuanika karafuu katika majamvi na si katika mapaa ya nyumba au chini katika barabara.

"Karafuu ni zao la pili ukiacha vanila ambalo lina bei kubwa Zanzibar, hivyo hamasa ya wakulima imekuwa kubwa kutokana na bei nzuri ya zao hilo," alisema.

Pia alisema kutokana na bei nzuri ya zao hilo kumekuwa na changamoto ya wizi wa karafuu mashambani na kuna malalamiko mengi kutoka kwa wakulima kisiwani Pemba kuibiwa karafuu zao.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa biashara ya magendo ya karafuu imepungua kwa msimu wa mwaka huu na kuwataka wakulima na wanunuzi kuhakikisha wanafuata masharti ili kupata kiwango cha daraja la kwanza.

Kuhusu uzalishaji wa mafuta ya makonyo ya karafuu, alisema kwa msimu wa mwaka huu uzalishaji umesita kutokana na kuharibika kwa baadhi ya vifaa katika mashine ya utengenezaji wa mafuta, lakini mwanzoni mwa mwezi ujao, wanatarajia kiwanda hicho kitaanza kazi.

# Wahimiza mazoezi kuepuka maradhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kutenga muda maalum wa kufanya mazoezi ili kupunguza ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa mwongozo wa kuushughulisha mwili na mazoezi ya viungo ili kuimarisha afya, iliyofanyika katika Hoteli ya Verde, Mtoni Zanzibar.

Alisema kukosekana kwa muda wa kufanya mazoezi kunasababisha kuongezeka kwa maradhi mbalimbali ikiwamo kiharusi, figo kushindwa kufanyakazi na kupoteza viungo kutokana na ugonjwa wa kisukari pamoja na magonjwa mengine.

Hemed alisema mwongozo huo umetoa maelekezo ya kufanya mazoezi kwa makundi ya rika zote wakiwamo wazee, vijana, wajawazito, watu wenye ulemavu pamoja na kugusia suala la matumizi ya lishe bora kwa mlo uliokamilika.

Alisema serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa elimu ya afya na imeongeza vituo vya afya kutoka vinane hadi 53, hivyo aliwakumbusha wananchi kuwa na tabia ya kufika katika vituo hivyo kwa ajili ya kujua afya zao.

Makamu wa Pili huyo alitoa wito kwa Wizara ya Afya na taasisi zinazohusika na michezo, kusimamia mwongozo huo kupitia viongozi wa vikundi vya mazoezi na makundi mbalimbali ili wananchi kufaidika vyema na mwongozo huo. Pia aliagiza shule zote za msingi na sekondari pamoja na vyuo vikuu kuandaa na kuendelea kusimamia muda wa kuushughulisha mwili na kufanya mazoezi kwa wanafunzi ili kukuza afya zao kwa kufahamu kuwa afya imara huongeza ufahamu.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto. Nassor Ahmed Mazrui, alisema mwongozo huo utasaidia wananchi kujua aina ya mazoezi wanayotakiwa kufanya kwa mujibu wa mahitaji ya hali za afya zao.

Aliishauri Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kutenga maeneo ya michezo katika nyumba za maendeleo zinazoendelea kujengwa nchini ili kutoa fursa kwa wananchi kutumia maeneo hayo kuushughulisha mwili na mazoezi. Akisoma risala, Dk. Lulu Omar kutoka Kitengo cha Maradhi Yasioambukiza Zanzibar, alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliopita, kumekuwa na ongezeko la Watanzania kupata magonjwa yasiyoambukiza na hadi mwaka jana, wagonjwa walifikia milioni 4.8 ikiwa ni ongezeko la asilimia 41 ya wagonjwa hao.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2008, magonjwa hayo yanachangia zaidi ya vifo milioni 41 kwa mwaka ambayo sawa na asilimia 71 ya vifo vyote vinavyotokea duniani.


ICB INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK

## TARIFFS GUIDE - EFFECTIVE FROM OCTOBER 2021

DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014

| MONTHLY MEINTENANCY FEE | TZS | USD | EURO | GBP |
|---|---|---|---|---|
| ICB Savings Account | 2,000 | 1.5 | 1.5 | 1.5 |
| ICB Salary Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Staff Savings Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| Al-Wadiyah Savings Account | Free | Free | Free | Free |
| ICB Lenga (Goal ) Account | Free | Free | Free | Free |
| ICB Wazee (Senior Citizen) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| ICB Premier Savings Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| ICB Chuo (Students) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| ICB Premier Current Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| ICB Current Account - Corporate | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| ICB Current Account -Personal | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| **MINIMUM OPENING BALANCE** | | | | |
| ICB Savings Account | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| ICB Salary Account | - | N/A | N/A | N/A |
| ICB Chuo (Students) Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| ICB Staff Savings Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| ICB Current Account -Personal | 50,000 | 50 | 50 | 50 |
| ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| ICB Premier Savings Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| ICB Current Account - Corporate | 100,000 | 100 | 100 | 100 |
| ICB Lenga (Goal ) Account | 20,000 | 100 | 100 | 100 |
| Al-Wadiyah Savings Accounts | 20,000 | N/A | N/A | N/A |
| **MINIMUM OPERATING BALANCE** | | | | |
| ICB Savings Account | 5,000 | 100 | 100 | 100 |
| ICB Salary Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Chuo (Students) Account | - | N/A | N/A | N/A |
| ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | - | N/A | N/A | N/A |
| ICB Current Account -Personal | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| ICB Premier Savings Account | 500,000 | 500 | 500 | 500 |
| ICB Current Account - Corporate | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| ICB Lenga (Goal ) Account | 20,000 | 100 | 100 | 100 |
| Al-Wadiyah Savings Accounts | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| **EXTRA CHARGE ON TRN BELOW MINIMUM BALANCE** | | | | |
| ICB Savings Account | 600 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| ICB Salary Account | 600 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Chuo (Students) Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| ICB Wazee ( Senior Citizen) Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| ICB Staff Savings Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| ICB Current Account -Personal | 600 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Premier Current Account | 5,000 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| ICB Premier Savings Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Current Account - Corporate | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Lenga (Goal ) Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| Al-Wadiyah Savings Accounts | N/A | N/A | N/A | N/A |
| **CASH WITHDRAW FEES** | | | | |
| Cash withdraw at the counter (All Current accounts): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 2000 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS120,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| Cash withdraw at the counter (All Savings accounts except ICB Chuoand Lenga Account): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 1500 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS 170,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| premature withdrawal and withdraw more than 3 per quarter | 1% charge of the principal amount | 1% charge of the principal amount | 1% charge of the principal amount | 1% charge of the principal amount |
| **FUND TRANSFERS/REMITTANCES** | | | | |
| Internal Transfers within ICB Bank | Free | Free | Free | Free |
| Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | Up to USD50,000.00 charge is USD50 | | |
| Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | above USD50,000.00 charge is USD75 | | |
| Inward Transfers (TT, SWIFT) | Free | USD 11.8 | | |
| Amendment of TISS, SWIFT Message | 11,800 | USD 11.8 | | |
| Amendment of TT, SWIFT Message | N/A | USD 20 | | |
| TISS | 11,800 | USD 11.8 | | |
| EFT (Bulk Payments): Out&Inward/salary processing fee | 3,000 per transaction | USD 2 per transaction | | |
| Stop Payments (TISS/EFT/SWIFT) | 20,000 | USD 20 | | |
| **CASH DEPOSIT** | | | | |
| ICB Accounts | Free | Free | Free | Free |
| ICB Agency Banking | Free | N/A | N/A | N/A |
| Bulk Cash | Free | Free | Free | Free |
| Deposit of Coins | 0.1% of the Amount | N/A | N/A | N/A |
| Small Denomination (1, 5, 10, and 20) | N/A | 5% of the Amount | 5% of the Amount | 5% of the Amount |
| **BALANCE ENQUIRY /STATEMENT** | | | | |
| ICB ATM Balance Enquiry | 300 | N/A | N/A | N/A |
| Balance Enquiry - POS | 300 | N/A | N/A | N/A |
| Balance Enquiry Within Banking Hall | 500 | Free | Free | Free |
| ICB Internet Banking | Free | Free | Free | Free |
| ICB Agency Banking | 500 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Mobile (APP) | Free | Free | Free | Free |
| interim statement | 1000 per page | 1 per page | 1 per page | 1 per page |
| Monthly statement & E-statement | Free | Free | Free | Free |
| **CHEQUE DEPOSIT** | | | | |
| Cheque From other Banks | Free | Free | Free | Free |
| Outward Special Clearance – Local Settlement | 53,100 | 52.8 | 46 | 39.5 |
| Inward Clearing | 1,000 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| Unpaid Cheque (Refer to drawer) | 35,000 | 20 | 20 | 20 |
| Unpaid Cheque (Refer to drawer) | 50,000 | 1.5% Min 59 Max 118 | 1.5% Min 59 Max 118 | 1.5% Min 59 Max 118 |
| **CHEQUE BOOK** | | | | |
| Cheque Book 100 Leaves | 100,000 | 50 | 50 | 50 |
| Cheque Book 50 Leaves | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Stop payment order per leaf; Reported Lost/Stolen Cheque Book/leaf (per notice | 35,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| **BANKERS CHEQUE** | | | | |
| Commission per issued Cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| Cancellation of Banker's cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| **STANDING INSTRUCTIONS** | | | | |
| SI - Set up/Amendment/closure | Free | Free | Free | Free |
| SI-Execution per Entry within ICB | Free | Free | Free | Free |
| SI-Execution per Entry outside ICB | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Unpaid SI due to Insufficient funds | Free | Free | Free | Free |
| **ATM/ DEBIT CARDS** | | | | |
| **ATM Card issuance fee** | | | | |
| ICB Master Debit Card | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| ICB Virtual Master Card | 3,400 | 1 | 1 | 1 |
| Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| **ATM Card replacement fee** | | | | |
| ICB Master Debit Card | 16,000 | 7 | 7 | 7 |
| ICB Virtual Master Card | 3,500 | 1 | 1 | 1 |
| Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| **Annual Card Maintenance** | | | | |
| ICB Master Debit Card | 9,500 | N/A | N/A | N/A |
| ICB Virtual Master Card | 35,000 | N/A | N/A | N/A |
| Umoja Switch Card | 11,800 | N/A | N/A | N/A |
| **ATM Transaction fee** | | | | |
| ATM card activation | Free | | | |
| Blocking/Hotting ATM card | Free | | | |
| Umoja ATM Cash Withdrawal | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| Umoja ATM Interbank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| Umoja ATM Intrabank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| Umoja ATM Transfers to Card-Less - (Remmitances) | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| Umoja ATM Balance Inquiry | 300 | N/A | N/A | N/A |
| Umoja ATM Mini Statement | 300 | N/A | N/A | N/A |
| POS Withdrawal up to TZS 20,000,000 | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| ATM Cash Withdrawal fee per transaction — Mastercard local | 4,000 | Local trn < USD15 0.5%: Local trn >USD15 - 1.1% : Cross- border 1.6% | | |
| ATM Cash Withdrawal fee per transaction — Mastercard International | 8,000 | | | |
| **INTERNET/ MOBILE BANKING** | | | | |
| Registration | Free | Free | | |
| Monthly Service Fee (Corporate) | 15,000 | USD 8 | | |
| Monthly Service Fee (Personal) | 7,000 | USD 4 | | |
| Funds Transfer between Selcom managed banks | TZS 500 | | | |
| Funds Transfer from Bank account to agents | TZS 500 | | | |
| NHC payments | TZS 1,000 | | | |
| Selcom Card funds transfers | TZS 500 | | | |
| TANESCO Postpaid Electricity Bill payment | Free | | | |
| TFDA- Certification application fee payment | TZS 1,000 | | | |
| Transfers through ICB Internet Banking | TZS 1,000 | | | |
| Transfers through Internet Banking File Upload Within | TZS 500 | | | |
| Transfers through Internet Banking File Upload TISS | TZS 5,000 | | | |
| Transfers through Internet Banking File Upload EFT | TZS 1,000 | | | |
| Transfers through Internet Banking File Upload B2W | TZS 500 | | | |
| UTT investor payments | TZS 1,000 | | | |
| DSTV Payments | | | | |
| 1 - 200,000/- | TZS 1,000 | | | |
| 200,000.01 to 500,000 | TZS 2,000 | | | |
| 500,000.01 + | TZS 5,000 | | | |
| **GENERAL ACCOUNT OPERATIONS** | | | | |
| Confirmation of Balance and Audit Statement | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| Salary processing manually per entry | 500 | N/A | N/A | N/A |
| Salary and Bulk payments outside the Bank | 3,000/transaction plus transfer fee | N/A | N/A | N/A |
| Advisory service - charged per advice | 2,500 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| Vouchers - Information less than one year | 15,000 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| Salary Alert per message | 118 | N/A | N/A | N/A |
| Court Order Closing of Account | Free | Free | Free | Free |
| Deliberate closing of Corporate account | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| Deliberate closing of Personal account | 11,800 | 5 | 5 | 5 |
| **Cash Change** | | | | |
| Cash Coins per bag of TZS 100,000 | 1,180 | N/A | N/A | N/A |
| **BONDS & GUARANTEE** | | | | |
| Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| Perfomance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| Extentions | 1.42% Per Quarter | | | |
| Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| Cancellations of guarantees if not Returned | 20000 | | | |
| **ADVANCED PAYMENT GUARANTEE** | | | | |
| Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance swift charges | Usd 50 | | | |
| **Export Collections (EC)-Outwar Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| Handling Commissions | 0.5% Min usd 100 | | | |
| Correspondance Commission-per tracer | Usd 50 | | | |
| Courier Charges | Usd 100 | | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

| | | |
|---|---|---|
| Villy Vellayappan | Chief Executive Officer | 26.10.2021 |
| George Msambazi | Head of Finance | 26.10.2021 |
| John Mwakasonda | Head of Internal Audit | 26.10.2021 |

HABARI KITAIFA

# Wateja kujishindia mamilioni kupitia simu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya Halotel jana imesaini mkataba wa ubia wa kimkakati na Dunia Investment ambao utawapa fursa wateja wake kujishindia mamilioni ya fedha na zawadi mbalimbali kupitia kampeni ya 'Play & Win'.

Mkataba huo ulisainiwa kati ya Mkuu wa Huduma na Mahusiano kwa Wateja wa Dunia Investment, Kobus Schoeman na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Halopesa, Magesa Wandwi.

Katika ubia huo kampuni hizo mbili zinakusudia kuwazawadia wateja wake fedha na zawadi mbalimbali kila siku, wiki na mwezi kupitia michezo itakayoendeshwa kupitia Halopesa.

"Ni hatua nyingine ya ubunifu kutoka Halopesa kufikisha thamani hiyo ya mtindo wa maisha kwa wateja wetu wote nchini," alisema Magesa.

Pia, alisema ubia huo wa kimkakati kati ya Dunia Investiment na Halopesa unaowezeshwa na Axieva Africa una lengo la kuzindua aina mbalimbali za michezo ya kubahatisha nchini na kuwawezesha wateja kutumia huduma zinazotolewa na kampuni hiyo.

Kwa upande wake, Schoeman alisema michezo na burudani ni sehemu asili ya utamaduni wa Kiafrika na kwamba kwa ushirikiano huo wanakusudia kuleta utamaduni huo kwenye simu ya mkononi.

"Tuna hakika kwamba, wateja zaidi wa Halopesa watafurahia huduma ya Play & Win na wengine zaidi watajiunga ili kufurahia faida za huduma hiyo," alisema.




Naibu Mkurugenzi wa Halopesa, Magesa Wandwi (kulia), na Mkuu wa Huduma ya Mawasiliano kwa Wateja wa Dunia Investiment, Kobus Schoeman, wakitia saini mkataba wa ushirikiano katika ofisi za makao makuu ya Halotel ikiwa ni uzinduzi wa huduma ya 'Pay and Win'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu waaswa kuhusu maadili

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) ngazi ya Taifa kimewataka walimu wa Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani kutekeleza wajibu wao ili kuepukana na hatua mbalimbali za kinidhamu.

Akifungua mafunzo ya siku mbili kwa viongozi wa CWT Wilaya hiyo, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa ya CWT, Harbert Ngimi, aliwataka walimu kuepukana na tabia ya kufanya mapenzi na wanafunzi ili kuepuka mkono wa sheria ambao utasababisha wapotee kwenye ajira zao na kuteseka sambamba na familia zao.

Aidha, Ngimi ambaye ni Mwenyekiti mstaafu wa CWT Wilaya, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupandisha madaraja walimu kote nchini, huku akiwataka waongeze juhudi katika utendaji kazi wao kama shukrani.

Katika hatua nyingine, aliwataka walimu wajenge ushirikiano na viongozi wao wa CWT sambamba na kuwa wasikivu kwenye mafunzo ili yalete tija.

"Walimu mnatakiwa kujenga ushirikiano na viongozi wa CWT ikiwamo na kuwa wasikivu katika mafunzo hayo ya siku mbili," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Chama hicho Wilaya, Joseph Awino, aliupongeza uongozi wa CWT Taifa kwa udhamini wa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa ofisi yao.

**Akifungua mafunzo ya siku mbili kwa viongozi wa CWT Wilaya hiyo, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa ya CWT, Harbert Ngimi, aliwataka walimu kuepukana na tabia ya kufanya mapenzi na wanafunzi ili kuepuka mkono wa sheria ambao utasababisha wapotee kwenye ajira zao na kuteseka sambamba na familia zao.**

# Waziri Jafo apigia debe hifadhi za Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewaita watu wa pande zote za dunia kutembelea hifadhi za taifa ambazo zimejaa vivutio mbalimbali vya utalii.

Aliyasema hayo katika hotuba yake aliyoitoa katika mkutano mkubwa wa nchi za mashariki ya kati wa 'Middle East Green Initiative' (MGI) 2021 uliofanyika Riyadh, Saudi Arabia. Jafo alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema dunia inapaswa kuja Tanzania kuona ilivyo makini katika kuhifadhi ambapo zaidi ya asilimia 32 ya eneo lake limehifadhiwa na kutaja hifadhi hizo kuwa ni Serengeti, Nyerere, Ngorongoro, Ruaha, Kilimanjaro na visiwa vya karafuu vya Zanzibar.

Jafo alisema Tanzania imeongeza uwekezaji kwenye nishati ya umeme kwa kujenga bawawa lenye uwezo wa kuzalisha umeme wa Megawati 2,115, hivyo kuifanya nchi kuwa na umeme wa uhakika.

"Leo nimejifunza kuwa lengo la MGI si tu kuongeza jitihada za kutunza mazingira kwa ukanda wa Mashariki ya Kati, lakini umeweka pamoja watoa uamuzi kutoka serikalini, sekta binafsi na wahisani ili kuweka mipango na kuitekeleza kwa ajili ya maendeleo endelevu," alisema.

Waziri Jafo alimshukuru Mfalme Mohamed Bin Salman na Waziri Mkuu wa Saudi Arabia kwa kumwalika Rais Samia kwenye mkutano huo ambao aliuelezea kwamba ni muhimu kwa ajili ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Pia Waziri Jafo alisema uchumi wa kijani ni ule unaozingatia maslahi mapana ya jamii, ukuaji wa uchumi na mazingira endelevu na kwamba ni njia ambayo ni rahisi kwa maendeleo endelevu ambapo suala la uhifadhi wa mazingira linakuwa kipaumbele.

Alisema serikali ya Tanzania inajitahidi kuboresha mfumo wa usafirishaji kwa kuanzisha usafiri wa haraka yaani Bus Rapid Transit (BRT) katika Jiji la kibiashara la Dar es Salaam ikiwa ni jitihada za kupunguza uchafuzi wa mazingira.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### POGBA AMPUUZA SOLSKJAER

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 28, alimpuuza kocha Ole Gunnar Solskjaer baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu katika kichapo cha mabao 5-0 kutoka Liverpool Jumapili na Mfaransa huyo amesimamisha mazungumzo ya mkataba mpya wa kusalia klabuni hapo. ***(Sun)***

### ROBERTO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wanajiandaa kupambana na Manchester City katika mbio za kumsajili kama mchezaji huru mlinzi wa Hispania, Sergi Roberto, 29, kutoka Barcelona. ***(Fichajes, via talkSPORT)***

### DE BEEK AKATAA RAIOLA

KIUNGO wa Manchester United, Donny van de Beek, amemkataa wakala wa soka Mino Raiola baada ya kumwomba Mholanzi huyo mwenye miaka 24 awe wakala wake mpya. ***(Mike Verweij, via Express)***

### CHELSEA YAITIWA DE LIGT

CHELSEA imepewa ofa ya kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Matthijs de Ligt, 22, wakati huu Juventus ikitaka kupunguza kiwango cha mishahara inayotoa kwa wachezaji. ***(Goal, via Star)***

### UTD NA ORODHA YA MAKOCHA

KLABU ya Manchester United ina orodha ya majina manne ya kumrithi kocha wake aliyekalia kuti kavu, Ole Gunnar Solskjaer, akiwamo Zinedine Zidane, Antonio Conte, kocha wa Leicester, Brendan Rodgers na wa Ajax, Erik ten Hag. ***(Sun)***

### HAG KULIPWA FEDHA NDEFU

NEWCASTLE wako tayari kumpa Ten Hag, 51, mshahara wa pauni milioni sita kwa mwaka baada ya kodi na kufanya marupurupu yote kufikia pauni milioni 11 kwa mwaka, lakini Mholanzi huyo amegoma kuondoka Ajax. ***(Mail)***

### BENITEZ KUNG'OLEWA EVERTON

NEWCASTLE pia haijakata tamaa kumrejesha kocha wake wa zamani, Rafael Benitez. Kwa sasa anainoa Everton. ***(Football Insider)***

### KLOPP ATAKIWA BARCA

BARCELONA bado wanamatumini ya kumpata kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp mwenye umri wa miaka 54, ili amrithi kocha wa sasa Ronald Koeman. ***(Sport)***

### POCHETTINO ATAJWA MAN U

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, 49, anasalia kuwa chaguo namba moja la Manchester United kumrithi, Ole Gunna Solskjaer. ***(Star)***

### ASHAWISHIWA KUONDOKA

Arsenal inahaha kumshawishi, William Saliba, 20, kurudi pale Emirates na wanaweza kulazimika kumuuza mlinzi huyo Mfaransa ameonyesha kiwango cha kuvutia pale Marseille anapocheza kwa mkopo. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND SASA KUFUNGIA MWAKA 2021 KITANDANI

Inawezekana mchezo wake dhidi ya Ajax Ligi ya Mabingwa Ulaya ulikuwa wa mwisho kwa...

**DORTMUND,** Ujerumani

HUENDA Erling Haaland atamaliza msimu huu bila kurejea uwanjani kwa sababu hakuna dalili za yeye kurejea dimbani hivi karibuni kutokana na straika huyo wa Borussia Dortmund kukabiliwa na jeraha la paja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amekuwa akisumbuliwa na jeraha la paja ingawa maendeleo yake hajaonyesha kama mshambuliaji huyo anaweza kurudi uwanjani.

**Kwa mujibu wa gazeti la Ujerumani la Bild, mshambuliaji huyo atakuwa nje ya uwanja hadi mwanzoni mwa mwaka 2022 kitu ambacho ni habari mbaya kwa mashabiki wa Dortmund.**

"Inawezekana mchezo wake dhidi ya Ajax kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ulikuwa wa mwisho kwa mwaka huu," alisema kocha wa Dortmund, Marco Rose akiiambia Bild.

Kukosekana kwa Haaland katika kikosi hicho litakuwa pigo kubwa kwa Borussia Dortmund ambao wanapambana katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Haaland alianza vema msimu kwa kufunga mabao 13 na kusaidia mabao mengine manne katika michezo 10 kwenye mashindano yote.

MECHI KALI
HOME
AWAY
LEVANTE
5.21 | 3.75 | 1.66
ATLETICO MADRID

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 619

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LIVER SASA KUKOSA MALIPO YA COUTINHO

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL sasa watakosa malipo ya pauni milioni 17 kutoka Barcelona kwa ajili ya mchezaji, Philippe Coutinho, kwa mujibu wa ripoti.

Awali kulikuwa na ripoti kuwa klabu ya Barcelona inapaswa kuwalipa Liverpool pauni milioni 17 kama Countinho atacheza mechi 100 klabuni hapo.


Nyota huyo wa Brazil ambaye aliwasili pale Camp Nou mwaka 2018 kwa dau linalotajwa kuwa pauni milioni 142, alikumbana na changamoto ya majeraha katika miaka yake takriban mitatu na nusu akiwa na Barcelona.

Hadi wakati huu, Philippe Coutinho amecheza jumla ya mechi 99 na jana Jumatano alitarajiwa kufikisha idadi ya mechi 100 akiwa na Barcelona kwenye mechi ya LaLiga dhidi ya Rayo Vallecano.

Licha ya kusemekana kuwa Liverpool wanapaswa kulipwa pauni milioni 17, gazeti la The Mirror limeripoti kuwa kipengele hicho hakikuwapo kwenye makubaliano ya awali ya klabu hizo mbili.

Akiwa na jumla ya mechi 99 kwenye hesabu zake, Coutinho amefanikiwa kufunga mabao 24 na kutoa asisti 14.

Staa huyo mkataba wake wa sasa unamalizika ndani ya kipindi cha misimu miwili ijayo.



# *Christensen: Nataka kubaki Chelsea*

**LONMDON,** England

MLINZI wa Chelsea, Andreas Christensen ameeleza shauku yake ya kutaka kubaki Chelsea, lakini hadi sasa bado hajafanya mazungumzo yoyote ya mkataba mpya na klabu hiyo.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark wa miaka minne unamfanya apokee kiasi cha pauni 140,000 kwa wiki, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja ambapo ingebidi mazungumzo yangeanza Agosti, lakini hadi sasa hakuna chochote kilichofanyika.

Christensen mwenye miaka 25 ameiambia BT Sport: "Najua sana mengi yanasemwa, siwezi sema sana, lakini nadhani ni vizuri."

"Najisikia furaha kuwa kwenye klabu hii, na najihisi Chelsea kuwa ndio sehemu sahihi kwa hapa Uingereza."

Christensen amecheza michezo 137 akiwa na Chelsea huku 27 ni msimu ulioisha chini ya Thomas Tuchel, wakifanikiwa kuchukua ubingwa wa Ulaya.

Pia safu ya ulinzi ya Chelsea ina walinzi wengine wanne ambao mikata ya inamalizika mwishoni mwa msimu huu pamoja na Christensen, wengine ni Antonio Rudiger, Azpilicueta na Silva.



,207,580

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/10/21 | 17:00 | Watford vs Southampton | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 02. 30/10/21 | 17:00 | Burnley vs Brentford | 2.80 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 30/10/21 | 17:00 | Derby vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 04. 30/10/21 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 05. 30/10/21 | 18:00 | Metz vs St Etienne | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 06. 30/10/21 | 19:30 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.79 | 3.38 | 2.49 |
| 07. 30/10/21 | 19:30 | Valencia vs Villarreal | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 31/10/21 | 15:00 | Angers vs Nice | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 31/10/21 | 16:00 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.67 | 2.97 | 2.92 |
| 10. 31/10/21 | 17:00 | Bordeaux vs Reims | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 11. 31/10/21 | 17:30 | Augsburg vs Stuttgart | 2.80 | 3.30 | 2.47 |
| 12. 31/10/21 | 19:30 | Aston Villa vs West Ham | 2.77 | 3.42 | 2.49 |
| 13. 31/10/21 | 22:45 | Roma vs AC Milan | 2.49 | 3.42 | 2.77 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 28 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4980 | Genclerbirligi vs Pendikspor | 1.50 | 3.86 | 5.79 |
| 14:00 | 5811 | Tuzlaspor vs Yeni Aksarayspor | 1.15 | 6.54 | 12.50 |
| 14:30 | 4187 | Sichuan Jiuniu vs Henan Jianye | 5.80 | 4.06 | 1.47 |
| 15:00 | 2387 | Gloria Buzau vs Dunarea Calarasi | 1.33 | 4.72 | 7.33 |
| 15:00 | 5885 | Dunajska Streda U19 vs Kosice U19 | 1.44 | 4.72 | 5.21 |
| 16:00 | 2070 | Prison Leopards vs Red Arrows | 2.42 | 2.67 | 3.20 |
| 16:30 | 5674 | ES Sahel vs Africain | 1.84 | 3.22 | 4.09 |
| 17:00 | 4349 | Atlas U20 vs Tijuana U20 | 1.38 | 4.82 | 5.98 |
| 17:15 | 2609 | AL Urooba vs Al Sharjah SC | 4.15 | 4.15 | 1.62 |
| 17:15 | 4784 | Al Nasr Dubai vs Ittihad Kalba | 1.52 | 4.26 | 4.84 |
| 18:00 | 5567 | U Craiova SA vs Sepsi Osk | 3.50 | 2.96 | 2.12 |
| 18:05 | 1193 | AL Hazm vs Al Ittihad Jeddah | 4.25 | 3.95 | 1.72 |
| 18:30 | 2578 | Orlando Pirates vs Bloemfontein Celtic | 1.69 | 3.43 | 5.10 |
| 18:30 | 4299 | Ghazl EL Mahallah vs Al Masry Club | 4.34 | 3.25 | 1.86 |
| 19:00 | 1591 | Rukh Vinnyky vs Zorya Lugansk | 3.61 | 3.37 | 1.90 |
| 19:00 | 2375 | Amstetten vs Rapid Vienna | 5.41 | 4.54 | 1.45 |
| 19:00 | 2972 | Ascoli vs Spal | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 19:00 | 3037 | Brann vs Viking | 2.19 | 3.65 | 2.91 |
| 19:00 | 3297 | Brescia vs Lecce | 2.40 | 3.34 | 2.75 |
| 19:00 | 3704 | CSKA Sofia vs Arda Kurdzhali | 1.62 | 3.76 | 4.63 |
| 19:00 | 3740 | Alessandria vs Frosinone | 3.28 | 3.18 | 2.17 |
| 19:00 | 4776 | LASK Linz vs WSG Wattens | 1.53 | 4.15 | 5.02 |
| 19:30 | 3632 | FCB Magpies vs Lynx FC | 3.56 | 3.75 | 1.81 |
| 19:30 | 5368 | FC Metalist Kharkiv vs Kolos Kovalivka | 1.77 | 3.61 | 3.85 |
| 19:45 | 4752 | Ajax Amateurs vs Cambuur | 7.33 | 5.79 | 1.26 |
| 20:00 | 1559 | Celta Vigo vs Real Sociedad | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 20:00 | 2348 | Halmstads BK vs Orebro SK | 1.51 | 3.87 | 5.61 |
| 20:00 | 3381 | Norrkoping vs Mjallby | 1.83 | 3.48 | 3.82 |
| 20:00 | 3390 | IFK Goteborg vs Djurgardens IF | 3.04 | 3.38 | 2.13 |
| 20:00 | 4073 | Degerfors vs Elfsborg | 3.88 | 3.78 | 1.75 |
| 20:00 | 4941 | Le Mans vs Orleans | 2.22 | 3.23 | 3.08 |
| 20:15 | 5963 | FAR Rabat vs Wydad Casablanca | 3.66 | 3.28 | 1.92 |
| 20:30 | 4737 | Kazincbaricika SC vs Diosgyori Vtk | 4.15 | 3.71 | 1.70 |
| 20:45 | 2810 | Midtjylland vs Aalborg | 1.59 | 3.94 | 4.62 |
| 20:45 | 3491 | Adana Demirspor vs Nigde Bld | 1.38 | 4.23 | 7.31 |
| 21:00 | 2360 | Granada vs Getafe | 2.61 | 2.86 | 3.06 |
| 21:00 | 3467 | Cercle Brugge vs KVK Tienen | 1.21 | 6.27 | 9.79 |
| 21:00 | 4957 | Sarpsborg vs Valerenga | 2.41 | 3.44 | 2.71 |
| 21:00 | 5039 | Politehnica Timisoara vs Rapid Bucuresti | 3.73 | 3.25 | 1.93 |
| 21:30 | 1016 | Perugia vs Reggina | 2.21 | 3.13 | 3.23 |
| 21:30 | 2401 | Crotone vs Benevento | 2.60 | 3.29 | 2.55 |
| 21:30 | 3112 | Cremonese vs Pisa | 2.12 | 3.24 | 3.34 |
| 21:30 | 5855 | Como vs Pordenone | 1.94 | 3.29 | 3.83 |
| 21:30 | 5878 | Cittadella vs Parma | 2.44 | 3.25 | 2.76 |
| 21:45 | 3673 | Napoli vs Bologna | 1.33 | 5.41 | 8.02 |
| 21:45 | 3693 | KVC Westerlo vs Royal Antwerp | 3.56 | 3.75 | 1.86 |
| 22:00 | 1641 | Deportivo Pasto vs Atletico Huila | 1.62 | 3.59 | 5.04 |
| 22:00 | 5839 | Waalwick vs Willem II Tilburg | 2.37 | 3.38 | 2.65 |
| 22:15 | 2453 | Sporting Braga vs Pacos Ferreira | 1.43 | 4.60 | 7.00 |
| 22:30 | 2701 | Levante vs Atletico Madrid | 5.21 | 3.75 | 1.66 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# ZIDANE HANA MPANGO NA UNITED



**PARIS,** Ufaransa

LICHA ya Zinedine Zidane kutajwa kama mmoja anayeweza kurithi mikoba ya Ole Gunar Solskjaer pale Manchester United, lakini yeye mwenyewe ameonyesha kuwa hana mpango huo.

Jina la Zidane limetajwa baada ya Man United kuchezea kichapo cha mabao 5-0 kutoka kwa Liverpool kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumapili.

Lakini kwa mujibu wa Jarida la France Football, Zidane mwenyewe hana mpango huo na wala hafikirii kuichukua nafasi hiyo.

Ripoti hiyo imesema kwamba, Zidane kwa sasa akili yake inawazia kuifundisha timu ya Taifa ya Ufaransa au klabu ya PSG.

United wanaendelea kukumbana na changamoto ya kurejea katika kiwango bora kwenye mashindano yote, Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya maboresho makubwa ya kikosi yaliyofanyika msimu wa majira ya joto.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa na uongozi wa Man United, klabu hiyo haitarajii kumfukuza Solskjaer hivi karibuni.




# Ramos fiti kuanza kuichezea PSG

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain imethibitisha kuwa Sergio Ramos anatarajia kujiunga kwenye mazoezi ya kikosi cha kwanza wiki ijayo baada ya kupona kutoka majeraha ya kigimbi, lakini Marco Verratti atakuwa nje ya dimba kwa karibia mwezi mmoja.

Ramos alijiunga na PSG kwa uhamisho huru kutoka Real Madrid kipindi cha majira ya joto, baada ya kutumia misimu 16 kule kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Mlinzi huyo mzoefu amejiunga na kikosi hicho pamoja pale kwenye dimba la Parc des Princes, akiwa pamoja na Lionel Messi, Gianluigi Donnarumma, Georginio Wijnaldum na Achraf Hakimi.

Lakini Ramos bado hajacheza mchezo wowote tangu kujiunga na PSG baada ya kuumia kigimbi mwishoni mwa Julai.

Lakini sasa PSG imethibitisha kwamba, Ramos atajiunga na mazoezi ya kikosi cha kwanza baada ya kupona ili aweze kuanza kuichezea timu hiyo.

"Sergio Ramos alikuwa kwenye programu maalumu na timu ya madaktari na sasa ameruhusiwa kuanza mazoezi," ilisema taarifa ya klabu hiyo kupitia kwenye tovuti yake.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 28, 2021

Nipashe



Haaland kufungia mwaka kitandani UKURASA 21

**HONGERENI...**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, baada ya kupokea Kombe la Ubingwa wa Cosafa na kuwakabidhi hati za viwanja katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nabi: Hesabu Yanga, Azam pasua kichwa

## ●●● Akiri mechi ngumu lakini pointi tatu muhimu, wapinzani wao wanacheka tu kurudishwa 'gemu' kwa...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

ZIKIWA zimebaki siku mbili kabla ya Jumamosi Yanga kuikaribisha Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kocha Mkuu wa timu hiyo mwenyeji, Nasreddine Nabi, amesema mchezo huo ndio kitu pekee kinachomuumiza kichwa kwa sasa.

**Miamba hiyo itakutana Yanga ikiwa nafasi ya pili katika msimamo baada ya kuvuna pointi tisa sawa na Polisi Tanzania iliyopo kileleni kutokana na kuizidi kwa tofauti kubwa ya mabao ya kufunga, wakati Azam ikiwa na alama nne, wakati huu kila moja ikiwa imeshuka dimbani mara tatu.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Nabi alisema kikubwa anachohitaji ni pointi tatu, na lazima vijana wake wavuje jasho katika kuzipambania ndani ya uwanja, jambo ambalo anaona linawezekana kutokana na ubora wa kikosi chake.

Alisema ana imani na vijana wake kwa sababu hadi sasa hawajapoteza mchezo wowote, hivyo watahakikisha wanaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa kwa sababu unapozitaja timu nne bora kwenye Ligi ya Tanzania, lazima utaigusa Azam FC.

"Hawajaanza vizuri, lakini hawa ni washindani kwenye mbio za ubingwa, mechi itakuwa ngumu kwetu, nimewaona walivyocheza na wao pia wametuona, nadhani itakuwa mechi ya mbinu na kiufundi zaidi ingawa nina matumaini ya kushinda," alisema Nabi.

Alisema wanaendelea na mazoezi kujiandaa na mchezo huo na wakipambana kusahihisha baadhi ya mapungufu ambayo wameyaona kwenye mechi zao zilizopita.

Wakati Nabi akisema hayo, nahodha wa Azam FC, Sospeter Bajana, amesema wamefurahi kusikia mechi yao dhidi ya Yanga imerudishwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, badala ya Sheikh Amri Abeid mjini Arusha kama wenyeji wa mchezo huo walivyosema hapo awali.

Vingozi wa Yanga, ambao ni wenyeji wa mchezo huo, awali walitangaza mechi hiyo kuihamishia Arusha, lakini baadaye wakatangaza kuirudisha Dar es Salaam.

"Mimi kama nahodha kwa niaba ya wachezaji wenzangu, tumefurahi sana mechi kurudishwa kwa Mkapa, kwa sababu ni uwanja mzuri sana. Mechi hii ni kubwa kama hizi ni lazima zichezwe kwenye uwanja mzuri.

"Tuaamini sasa mechi itakuwa nzuri na ngumu kwa sababu wachezaji wataonyesha ufundi wao, itakuwa mechi bora, ila tu niwaambie Yanga watakuwa na mechi ngumu sana siku hiyo," alisema nahodha huyo.

Kuhusu mechi hiyo kurudishwa Uwanja wa Benjamin Mkapa badala ya Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, Msemaji wa Yanga, Haji Manara, alisema kuwa Kocha Mkuu, Nabi ndiye aliyeshauri irudishwe Dar.

"Viongozi walitaka mechi ichezwe Arusha, lakini kocha akasema kwa mpira anaofundisha kwa pasi za chini, mechi ni lazima ichezwe Dar. We fikiria zile pasi za akina Aucho, Fei Toto, Bangala halafu mpira ukachezwe kwenye uwanja ambao si rafiki, hapana, kocha akaona bora irudishwe Dar es Salaam," alisema.

# Rais Samia awapa Twiga Stars viwanja

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amewazawadia viwanja wachezaji wote wa timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, ikiwa ni pongezi kwa kutwaa Kombe la COSAFA, Oktoba 9, mwaka huu nchini Afrika Kusini kwa kuichapa Malawi bao 1-0 kwenye mechi ya fainali.

Rais Samia aliwakabidhi hati za viwanja wachezaji hao katika hafla ya kukabidhiwa kombe hilo, iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana mchana, ambapo aliwataja kinadada hao kuwa ni mashujaa huku akiwataka kuendelea na kazi hiyo ya kuleta makombe nyumbani, kuipa sifa nchi na kuitangaza kimataifa.

"Nitawapatia watoto wangu viwanja vya kujenga nyumba zao. Kwa bahati mbaya au nzuri viwanja vyote vitakuwa kule ambako mama yenu nitakakokaa Dodoma. Najua baadhi yenu itakuwa shida kujenga Dodoma, lakini leo pokeeni viwanja, tutajua nini cha kufanya.

"Kuna maisha baada ya soka, ni mchezo unaotumia nguvu, baadaye zinaisha, lazima tuwatengenezee maisha. Wakisimamisha nyumba zao watahangaika na mambo mengine, mtu hupata heshima unapokuwa na nyumba yako, kala ugali na ndimu ni kwake, hayupo nyumba ya kupanga wenzake wakamsema kuwa Amina amekula ugali na ndimu," alisema Rais Samia.

Rais aliwasifu wachezaji hao kwa uchezaji wao, kwani alisema alikuwa akishuhudia jinsi walivyokuwa wakicheza na kwa kutwaa ubingwa kumemfanya kutembea kifua mbele.

"Pamoja na kwamba soka la wanawake limeanza hivi karibuni, lakini mafanikio yenu yameanza kutetemesha wanaume. Mimi huwa nasema timu ya wanawake inafanya vizuri mara kadhaa, lakini hakuna anayesimama kuwasifu. Lakini timu ya wanaume ikifika nusu fainali tu, sifa zinapasua anga.

"Kwa mlichokifanya baada ya fainali, nikajiambia ipo haja ya kukaa nanyi kupata chakula cha mchana Ikulu, ili tuweze kupongezana, kubadilishana mawazo, lakini kuangalia tunawezaje kusonga mbele kwa mafanikio makubwa zaidi kwenye tasnia hii," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >